

# MUHURI WA PILI



Habari za jioni, wapendwa. Hebu sote na tusimame kidogo tuombe.

<sup>2</sup> Baba yetu wa Mbinguni, tumekusanyika tena katika kusanyiko hili tulivu, usiku huu, katika ibada ya Bwana. Nawe umeahidi kuwa po pote ambapo tungekutanika pamoja, kadiri ya wawili ama watatu wetu, kwamba ungekuwa kati yetu. Nasi tunaweza kuwa na hakika kuwa Wewe uko hapa, kwa kuwa tumekusanyika katika Jina Lake.

<sup>3</sup> Sasa tunaomba, Baba, ya kwamba—ya kwamba utakuja usiku huu na utavunja Muhuri huu wa Pili kwa ajili yetu. Na kama vile m—mtunga mashairi alivyosema, angetaka kutazama ng'ambo ya pazia la wakati. Na hiyo ndiyo shauku yetu, Bwana, ni kuninii tu—kutazama tu ng'ambo na kuona kile kilichoko huko mbele. Nasi tunaomba ya kwamba yule Mwana-Kondoo ambaye amechinjwa, atakuja kati yetu sasa na kuvunja Muhuri huu, na—na kutufunulia sisi huo, mambo tunayohitaji kuona.

<sup>4</sup> Kama kuna wengine hapa, Bwana, ambao hawajaingia katika ushirika huu mkuu katika Kristo. Tunaomba ya kwamba, usiku huu, ya kwamba watafanya uamuzi huo wa Milele, wajazwe na Roho wa Mungu.

<sup>5</sup> Kama kuna ye yote aliye mgonjwa, Baba, tunaomba ya kwamba utawaponya. Kuna vitambaa vingi vilivyowekwa hapa ambavyo nimeviwekea mikono yangu, kwa ukumbusho wa—wa Biblia, wa Mtakatifu Paulo, ambapo walichukua toka mwilini mwake vitambaa na aproni. Pepo wachafu wakawaacha watu, nao wakaponya.

<sup>6</sup> Tunaona Kuja kwa Bwana kunakokaribia. Tunajua ya kwamba wakati unakaribia. Mambo haya yamerudi tena Kanisani, baada ya miaka elfu moja na mia tisa.

<sup>7</sup> Sasa tunaomba, Baba, ya kwamba utatupa mambo haya tunayokuomba. Mtie nguvu mtumishi Wako, na wasaidie watumishi Wako kila mahali, Bwana, na hasa sisi tuliokusanyika hapa usiku huu, ili tuweze kulipokea Neno. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>8</sup> Ni vizuri kweli kurudi hapa katika nyumba ya Bwana tena usiku huu. Nami najua wengi wenu sana mmesimama, na—nasikitika kuhusu jambo hilo, lakini ni vigumu sasa hivi sisi kufanya jambo lo lote la zaidi. Tu—tumeninii—tumeninii kanisa kama tu... tumelipanua kufikia ambapo tunaweza kuingiza ninii tatu au nne, watu mia tatu au mia nne zaidi ndani. Bali katika mikutano maalum ya namna hii, hu—huwa kuna msongamano mkubwa zaidi kidogo.

9 Sasa, loo! nina wakati mzuri sana kwa kweli, kuomba, na kusoma kwa undani Mihuri hi—hii. Ninatumaini ninyi nanyi ni vivyo hivyo, pia. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nina—nina hakika mnafanya vivyo hivyo. Na ikiwa inamaanisha kwenu sawa na inavyomaanisha kwangu, bila shaka ni . . . mna wakati mzuri sana. Nami nina ninii . . .

10 Nataka kumpigia simu rafiki yangu msichana, baada ya ibada. Na hii ni siku ya kuzaliwa kwake. Yeye ana miaka kumi na miwili leo, Sarah, binti yangu. Na baadaye, basi, kesho kutwa, itanibidi kupiga simu nyingine, kwa sababu ni sikukuu ya kuzaliwa kwa Becky.

11 Na sasa, usiku huu, tunajifunza kwa undani Muhuri huu wa Pili. Na katika hii Mihuri minne ya kwanza kuna wapanda farasi wanne. Nami nawaambieni, leo jambo fulani lilitukia tena. Na, mimi—mimi, jambo fulani ambalo mimi . . . Ninakwenda na kuchukua maandishi ya zamani niliyokuwa nayo, niliyohubiria, siku nyingi zilizopita, na nikaketi tu chini pale. Nami nikawazia, “Vema, ni—nilijitahidi sana nilivyoweza.” Na maandishi wengi na mambo mengi, basi nikawazia, “Vema, nitasoma kidogo, kisha nichunguze na nione jambo *hili* na *lile*.” Ndipo muda si muda wajua, mara jambo fulani linatendeka, na ni kitu tofauti kabisa na ilivyokuwa. Linatokea tu vinginevyo. Ndipo ninanyakua penseli upesi sana, na kuanza kuandika haraka niwezavyo, wakati Yeye akiwa angalipo.

12 Loo! ni jambo fulani tu lililotendeka yapata tu saa moja na nusu iliyopita. Nilikuwa nikimwambia Ndugu Woods, tulipokuwa tunakuja, dakika chache tu zilizopita. Jambo fulani tu, unajua. Unajua, kuna mambo mengi sana yanayotendeka, ambayo huwezi tu kuyasema, unajua. Lakini jambo fulani tu lilitukia tu hivi punde ambalo kwa kweli lilinisaidia sana.

13 Nina rafiki mahali fulani hapa katika jumba hili. Bila shaka, ninyi nyote ni marafiki zangu. Huyu—ndugu huyu ni Ndugu Lee Vayle. Yeye ni ndugu mpendwa, naye ni mjuzi kweli wa Maandiko. Dk. Vayle ni Mbatisti aliye na Roho Mtakatifu. Naye ni nanii . . . Sisemi hili kwa kumsifu, ninalisema jambo hili tu kwa sababu ninaliamini. Nadhani yeye ni mmojawapo wa wanafunzi waliosoma sana niwajuao, kati yetu. Naye ameniandikia kijikaratasi kidogo hapa hivi punde, na kikaletwa hapo ndani na Billy. Na Billy alipata shida ya kunisomea, mimi. Nami nafikiri . . . Sijakisoma, lakini nilikuwa ninataka tu kusema yale aliyosema hapa. Nami ndio nimekisoma sasa hivi, Ndugu Vayle, kama uko hapa. Nilisoma jambo hili yapata miezi sita iliyopita.

14 “Sina hakika,” yeye alisema. “Ndugu Bill, sina hakika, lakini ninaamini ya kwamba Polikapu alikuwa ni mwanafunzi wa Yohana Mtakatifu.” Hiyo ni kweli. Ndivyo alivyokuwa. “Nafikiri Ireneo alikuwa ni mwanafunzi wa—wa Polikapu.” Hiyo

ni kweli, sawa kabisa.” “Ireneo alisema, ‘Yesu atarudi—atarudi wakati mshiriki wa mwisho aliyeteuliwa wa Mwili wa Kristo atakapoingia.’”

<sup>15</sup> Huyu alikuwa ni Ireneo, yapata miaka mia nne kwenye . . . baada ya kifo cha Kristo. Yeye alisema, “Hapo wakati huu wa mwisho utakapofika . . .” Sasa, hiyo ni katika ka—kabla ya lile Baraza la Nikea. Enyi watu mlio hapa, mnaosoma Ma—Ma . . . kujifunza Maandiko, na kujifunza ninii . . . namaanisha, kujifunza historia ya Biblia, mnaona ya kwamba katika ninii la . . . la lile Baraza lililotangulia Nikea. Nami nafikiri ni kitabu cha kwanza ama cha pili, m—mtalipata humo. Na sasa, yeye aliona jambo hilo, miaka kadha iliyopita, hata akasema, “Hapo yule wa mwisho, wa mwisho—wa mwisho aliyeteuliwa, yule aliyeteuliwa.”

<sup>16</sup> Watu wanadhani ya kwamba uteuzi ni jambo ambalo limenini tu—ni jambo ambalo limebuniwa tu hapa hivi majuzi. Jamani! Hilo ni moja ya mafundisho ya zamani sana tuliyo nayo: kuteuliwa na kuitwa. Na kwa hiyo Ireneo, bila shaka, wale wanafunzi halisi wa Maandiko, daima waliamini katika kuteuliwa.

<sup>17</sup> Na kwa hiyo Ireneo alikuwa ni mmojawapo wa—wa malaika wa wakati wa kanisa, kama tulivyoona, kama tulivyojifunza. Tunaamini. Bila shaka, sasa, yote yalikuwa ni siri. Yote yako hapa, kabisa, yamefichwa papa hapa katika Mihuri hii, mnaona. Nazo zinapaswa kufunuliwa katika siku ya mwisho. Jinsi walivyoanza na Paulo, na—na Ireneo, na Martin, na kadhalika, wakaendelea, na wameendelea mpaka wakati wa mwisho.

<sup>18</sup> Na, sasa, tunatumaini sasa ya kwamba Bwana atatubariki katika jitihada zetu usiku wa leo. Sasa tumekuwa . . . Muhuri wa Kwanza, kweli niliufurahia huo. Muhuri wa Kwanza, zile baraka zilizoambatana Nao, kwangu mimi!

<sup>19</sup> Na sasa si—sitaki kuwaweka kwa muda mrefu sana. Lakini, mnaona, ni—nitaondoka sasa tena, katika masiku machache, na baada ya haya kwisha. Nasi hatuna budi kuvumilia kwa muda kidogo. Nami nafurahia . . .

<sup>20</sup> Ninamwona Ndugu Junior Jackson amesimama pale. Mimi . . . Nami nilidhani nilimwona Ndugu Ruddell, muda mchache uliopita, hapa mahali fulani. Na hao ndugu, hayo ni makanisa washiriki wenzetu na ambayo yamehudhuria, na mengineyo. Hakika tunalifurahia jambo hilo. Na ninamwona Ndugu Hooper, ninaamini, amesimama karibu na ukuta pale, kutoka Utica, kanisa lililoko kule. Na bila shaka tunathamini ushirikiano wenu wote mzuri katika jambo hili.

<sup>21</sup> Sasa, jana jioni, kama daima tunavyopendelea, katika kufundisha juu ya—juu ya ile ile Mihuri, tunaifundisha kwa njia ile ile mtu unayofanya juu ya—juu ya—juu ya zile nyakati za kanisa. Na wakati tulipomaliza kufundisha juu ya wakati wa

kanisa, wakati wa mwisho nilipozichora hapa mi—mimbarani, ubaoni, ni wangapi wanaokumbuka yaliyotukia? Yeye alishuka moja kwa moja, akaenda moja kwa moja kule nyuma ukutani, katika Nuru, na kuzichora, Mwenyewe, moja kwa moja pale ukutani, mbele yetu sote. Malaika wa Bwana alisimama papa hapa mbele ya watu mia kadha.

<sup>22</sup> Na sasa Yeye—Yeye anafanya jambo fulani la kimbinguni kweli kweli sasa, pia, na kwa hiyo tunatarajia tu mambo makuu. Hatujui. . . Unapenda kungojea tu hayo—hayo matarajio makubwa, hatujui tu litakalotukia tena, unajua, unaninii tu—unangojea tu. Haya, jinsi Mungu alivyo mkuu kwetu, na jinsi alivyo wa ajabu! Tunamfurahia sana!

<sup>23</sup> Sasa, aya ya 1 na ya 2, nitaisoma, kuweka msingi kidogo kwa namna fulani. Kisha tutachukua aya ya 3 na ya 4, kwa ajili ya Muhuri wa Pili. Halafu aya ya 5 na ya 6 ni Muhuri wa Tatu. Na ya 7 na 8 ni ile. . . Aya mbili kwa kila mpanda farasi. Na sasa nawatakeni mwangalie jinsi jamaa hawa. . . Kuhusu farasi huyu wa kijivu, labda. . . Huyu hapa anakuja, anaendelea tu kubadilika anapoendelea mbele.

<sup>24</sup> Na ndipo ule Muhuri mkuu, Muhuri wa mwisho kufunguliwa, Mungu akipenda, Jumapili ijayo usiku! Ambapo, jambo hilo lilipotukia, kulikuwa tu na ninii, jambo pekee lililotukia, “ilikuwa ni kimya Mbinguni kwa muda wa nusu saa.” Mungu atusaidie.

<sup>25</sup> Sasa nitasoma aya ya 3 sasa.

*Na alipoifungua muhuri ya pili, nikamsikia yule mwenye uhai wa pili akisema, Njoo uone!*

*Akatoka farasi mwingine, . . . (aya ya 4) . . . mwekundu sana, na yeye aliyempanda alipewa kuiondoa amani katika nchi, ili watu wauane, . . . watu wauane, naye akapewa upanga mkubwa.*

<sup>26</sup> Sasa, jambo la siri sasa, wakati yu—yule Mwenye Uhai alipomwambia Yohana, “Hebu njoo tu uone.” Naye hakuona ilikuwa ni kitu gani. Aliona mfano tu. Na mfano huo, sababu ya huo mfano. . . Alisema, “Njoo, uone,” lakini aliona mfano, ambao alikuwa auonyeshe kwa kanisa, katika njia ambayo wao wangangoja; mpaka itakapofikia kwenye wakati wa mwisho, na ndipo Muhuri huo ungefunguliwa.

<sup>27</sup> Sasa, kila mtu anaelewa na hilo sasa, mnaona, ile Mihuri itafunguliwa. Basi hivi ninyi hamna furaha kuishi katika siku hii? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hilo, mnaona, si hilo tu, enyi wapendwa, lakini daima kumbukeni sasa, Jumapili iliyopita asubuhi, katika ambalo jambo hilo lote liliwekewa msingi, urahisi! Mnaona? Rahisi, nyenyekevu, linatendeka kwa njia ambayo watu wanalipita tu na hata hawajui Hilo linatukia.

<sup>28</sup> Na, kumbukeni, tunakutazamia kule Kuja kwa Bwana, wakati wo wote. Na wakati sisi. . . Nilitoa tamshi, ya kwamba labda mimi Kunyakuliwa kutakuwa jinsi hiyo hiyo. Kutapita, kupite, na hakuna mtu atakayejua habari zake. Kutatukia tu namna hiyo. Unaona? Na kwa kawaida. . . Rudi tu nyuma upitie kwenye Biblia na uangalie jinsi linavyotukia namna hiyo. Unaona?

<sup>29</sup> Hata jambo kubwa kama kule kuja kwa Bwana Yesu, hakuna mtu aliyejua lo lote juu yake. Wao walidhania, “Huyo mwenda wazimu, mtu fulani.” Makanisa yalisema, “Ni mshupavu tu wa dini. Sisi. . . Yeye kweli ana kichaa.” Yasema, “Yeye ni mwenda wazimu.” “Tunajua wewe ni mwenda wazimu.” *Mwenda wazimu* maana yake ni “kichaa.” “Tunajua una pepo, na amekutia kichaa. Nawe ati unajaribu kutufundisha sisi? Wakati, Wewe ulizaliwa huko mitaani, isivyo halali. Sisi. . . Wewe ulizaliwa katika uasherati. Ati unajaribu kuwafundisha watu kama sisi, makuhani, na kadhalika, hekalu?” Vema, jamani, huko kulikuwa ni kuwatukana.

<sup>30</sup> Yohana alipokuja, alikuwa amenenwa habari zake, kote kote katika miaka mingi iliyopita, tangu Isaya mpaka Malaki. Hiyo ni miaka elfu moja mia mbili. . . ama miaka mia saba na kumi na miwili, aliyokuwa ameishaonwa na manabii, akija. Kila mtu alikuwa akimtazamia aje, akilitarajia jambo hilo wakati wo wote. Lakini jinsi alivyokuja, yeye alihubiri na kutimiza huduma yake, kisha akaenda Utukufuni.

<sup>31</sup> Wala hata mitume hawakujua jambo hilo, kwa maana wao walimwuliza. Walisema, “Sasa, kama—kama Mwana wa Adamu anaenda Yerusalemu, mambo haya yote, ya Yeye kutolewa dhabihu,” wakasema, “mbona Maandiko husema ya kwamba ‘Eliya hana budi kuja kwanza?’”

<sup>32</sup> Yesu akasema, “Amekwisha kuja tayari, wala hamkutambua hilo. Naye alifanya sawasawa na Maandiko yalivyosema atafanya. Nao walimfanyia sawasawa na yale aliyoandikiwa.” Unaona? Nao hawakuweza kufahamu hayo. Yeye akasema, “Ilikuwa ni Yohana.”

Na, ndipo, “Loo!” Unaona, wao—wao wakazinduka, katika jambo hilo. Wao. . .

<sup>33</sup> Na wakati, hata, hatimaye, baada ya mambo yote Yeye a—aliyokuwa amefanya, na ishara alizowaonyesha, na hata alikuwa amewaita. Kasema, “Ni nani kati yenu awezaye kunihukumu kwamba Mimi nina dhambi, kutokuamini? Kama sijafanya sawasawa kabisa na yale Maandiko yalivyosema kwamba huduma yangu itafanya nitakapokuja duniani, basi nionyesheni mahali ambapo nimetenda dhambi. Unaona? Ndipo nita—nitawaonyesha kile mnachopaswa kuwa, na hebu tuone kama mnaamini jambo hilo, au la.” Unaona? Angalirudi moja kwa moja na kusema, “Mlipaswa kuniamini Mimi nilipokuja.”

Hawakumwamini, unaona, kwa hiyo walitahadhari kumtegea, kwenye jambo hilo. Lakini Yeye alisema, “Ni nani kati yenu anayeweza kunihukumu Mimi juu ya kutokuamini? Unaona? Je! Mimi sikufanya jinsi vile ilivyotakiwa?”

<sup>34</sup> Na hata wale mitume, walipokuwa njiani wakienda, waliona mashaka. Tunajua vile Maandiko yasemavyo. Ndipo hatimaye, mwishowe, wakasema, “Sasa tunaamini. Tunaamini ya kwamba hakuna mtu anayepaswa kukwambia Wewe, kwa maana unajua mambo yote.”

<sup>35</sup> Sasa, laiti ningaliuona uso Wake. Hapana budi aliwaangalia, akasema, “Vema, sasa mnaamini? Hatimaye limewaelea.” Vema, halikupaswa kufahamika, labda, mpaka wakati huo, unaona. Na Mungu hufanya kila kitu sawasawa kabisa, unajua. Nininapenda kwa ajili ya jambo hilo.

<sup>36</sup> Lakini sasa tunafikiri juu ya wakati wetu sasa. Maana, nikiendelea kuzungumzia jambo hilo, hatutaingia kwenye Mihuri hii, kabisa.

<sup>37</sup> Na sasa, kumbukeni, ninapata maombi mengi ya kuwaombea wagonjwa. Na ninaombea ninii. . . wakati wote, kila ombi ninalopata, na kwa ajili ya vitambaa na kadhalika. Na kama tunaweza kumaliza Mihuri hii, mpaka ule Muhuri wa mwisho, Jumapili asubuhi tutaninii. . . Kama ikiwa ni mapenzi ya Bwana, tungetaka kuwa na ibada ya mtindo wa kale ya uponyaji hapa, wajua, ambapo unachukua tu asubuhi nzima kuwaombea wagonjwa. Nami ni—nina hakika kabisa utakuwa ni mkutano wa ajabu wa uponyaji. Unaona? Ninajisikia tu namna hiyo, unaona. Na kwa hiyo, si wa ajabu, lakini huenda ukawa wa ajabu kidogo kwa baadhi ya watu fulani, unaona, ninalomaanisha.

<sup>38</sup> Sasa, jinsi neema ya Mungu ilivyo kuu, kutufunulia sisi siri Zake katika siku hii! Sasa, sote tutaamini ya kwamba tunaishi katika siku ya mwisho. Tunaamini jambo hilo. Na kumbukeni, zile siri zilikuwa zifunuliwe katika siku ya mwisho. Na Yeye hufunua Neno Lake namna gani, siri Zake? Biblia ilisema. Mngetaka kusoma mahali Yeye anaposema jambo hilo? Hebu na tufungue tu tuone jinsi Yeye anavyofunua siri Zake.

<sup>39</sup> Sasa nataka msome Amosi. Fungueni Kitabu cha Amosi, nami nataka msome katika sura ya 3 ya Amosi, na aya ya 7. Vema. Nitasoma aya ya 6, pia.

*Je! tarumbeta. . . ilie mjini, na watu wasiogope? Mji utapatikana na hali mbaya, asiyoileta BWANA?*

*Hakika Bwana. . . hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri zake.*

<sup>40</sup> Sasa, katika siku za mwisho, sisi tunaninii. . . Imebashiriwa kwetu ya kwamba atainuka na—nabii.

41 Sasa, tunajua ya kwamba tumekuwa na wa kila aina. Sasa, ninatambua, baada ya kuangalia kila mahali usiku wa leo, ni—ninazungumza hapa ambapo wasomi wameketi, nami—ningetaka mnielewe. Nanyi mnatambua, kanda hizi zinapelekwa kote ulimwenguni, unaona, karibu tu ulimwengu mzima. Nami singewataka, kwa njia yo yote kutonini, mfikiri ya kwamba ninajaribu kuingiza namna fulani ya ma—madhehebu ya mablanketi ya Eliya ama majoho yake. Na vitu hivyo vyo—vyote, tumekuwa navyo vingi sana. Lakini, mnajua, vitu hivyo vyote ni utangulizi tu wa kile kilicho halisi kitakachokuja, kusudi viwapoteze watu.

42 Je! mlipata kujua tulikuwa na viongozi wa u—uongo walioinuka, masihi wa uongo, kabla ya kuja kwa Kristo? Je! si ninii. . . Yule mwalimu wa siku zile, yule mwalimu hodari sana, Gamalieli, wakati lile—lile swali lilipozuka juu ya kuwapiga watu hawa, na kadhalika, alisema, “Waacheni. Kama linatoka kwa Mungu, mbona, mtajikuta mnapigana na Mungu. Lakini kama si la Mungu. . .” Kasema, “Je! si paliinuka mtu, si muda mrefu umepita, na kuwapeleka watu mia nne jangwani, na kadhalika? Mambo hayo tunayo.” Ilikuwa ni nini? Yote yakitangulia Jambo lililo halisi wakati litakapokuja.

43 Sasa, unaona, Shetani huwainua hao. Angalia ujanja wa jamaa huyu tunayenena habari zake hapa, Shetani, ambapo tunamfunua papa hapa; tukimvua tu nguo, kwa Maandiko, na kukuwezesha uone yeye ni nani. Hilo ndilo ninii. . . linalopaswa kufanyika.

44 Na, mnakumbuka, yeye hajajaribu kuingia na kuwa mkomunisti, Shetani hajajaribu. Yeye ni mpinga-Kristo. “Anafanana sana, hata,” Yesu alisema, “angewapoteza walio Wateule. . .” Na hao ndio waliofichwa chini ya Mihuri hii, ambao majina yao yamo katika kile Kitabu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

45 Yeye ni jamaa mwerevu. Na wakati anapoona jambo hili likija, likitukia, ndipo anatupa kila kitu awezacho huko nje, apate kukivuruga kabla hakijafika pale. Je! mljua kutakuwako na makristo wa uongo watakaoinuka katika siku za mwisho? Hilo halina budi kufuata mara baada ya huu, baada ya Ujumbe huu mkuu ambao ndugu huyu atanena habari zake, ambaye atakuja kweli, ametiwa mafuta katika roho ya Eliya, mara moja.

46 Nao watamfikiria vibaya. Wengine wao watafikiri yeye ni Masihi. Lakini yeye atasema kwa uthabiti, “La.” Kwa sababu, haina budi kuwa ije kama Yohana.

47 Katika wakati wa Yohana Mbatizaji, wakati alipotoka akaenda kule kuhubiri, wao walimwambia, “Je! wewe ni Masihi? Wewe sie Yeye?”

48 Yeye akasema, “Mimi siye. Mimi sistahili kufungua viatu Vyake. Lakini na—nawabatiza kwa maji, bali Yeye atawabatiza

kwa Roho Mtakatifu.” Naye Yohana alikuwa na hakika sana ya kwamba Yeye alikuwa yuko duniani, akasema, “Yeye yuko miongoni mwenu, mahali fulani, sasa.”

<sup>49</sup> Lakini yeye hakumjua mpaka alipoona ile ishara ikishuka juu Yake. Ndipo, wakati alipoona ile Nuru ikishuka na kuenea kama hua, na kutua juu Yake, akasema, “Ni yule pale. Ni Yeye.” Lakini Yohana ndiye peke yake aliyeiona Hiyo, mnajua. Yohana ndiye tu aliyeisikia ile Sauti. Hao wote wengine pale, hakuna hata mmoja aliyeisikia.

<sup>50</sup> Lakini basi wakati yule mtumishi halisi, wa kweli anapokuja; kukiwako na maigizo yote ya jambo hilo, ni kwa maksudi ya kuhangaisha akili za watu. Shetani hufanya jambo hilo. Na wale wasioweza kupambua kweli na uongo, wanajikwaa na kuanguka tu. Lakini walio Wateule hawatakawazika; Biblia ilisema yeye hataweza kuwapoteza walio Wateule. Na sasa, kabla tu ya kule Kuja kwa Kristo, Biblia ilisema, “Makristo wa uongo watatokea, nao watadai kwamba wao ni Kristo, na watasema, ‘Tazama, watu wanasema Yeye yuko jangwani.’ Msiamini jambo hilo. ‘Tazama, Yeye yuko katika chumba cha siri.’ Msiamini jambo hilo.”

<sup>51</sup> “Kwa maana kama vile jua liangazavyo toka mashariki hadi magharibi, ndivyo Kuja kwa Mwana wa Adamu kutakavyokuwa.” Unaona? Naam, Yeye ata—ata—ataatokea, nalo litakuwa ni jambo la dunia nzima. Na sasa jambo hilo litaninii, sasa, bila shaka, wakati watakapogundua kwamba jambo fulani limetukia, unaona, basi wao wataninii . . . Sasa, kumbuka, jambo hilo litatukia mara baada ya kanisa kwenda Nyumbani, baada ya kunyakuliwa.

<sup>52</sup> Sasa kutakuwako na maigizo ya uongo, sikuzote, nasi hatutaki kuhusika na jambo lo lote kama hilo. La, bwana.

<sup>53</sup> Nami naamini, wakati mtu huyo atakapokuja, huyu ambaye ametabiriwa kuja, ninaonyesha jambo hilo tu kwa Maandiko peke yake, ya kwamba mtu huyo hana budi kuwa ni nabii. Hakika atakuwa ni nabii. Na ufunuo wa Mungu, kwa sababu Mungu . . . Neno la Bwana huwajia manabii Wake. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni . . . Na Mungu hawezi kubadilika, unaona. Kama angekuwa na utaratibu bora zaidi, Yeye ange—angeliutumia. Lakini Yeye—Yeye ana— . . . Yeye alichagua utaratibu bora zaidi ya wote hapo mwanzo.

<sup>54</sup> Ni kama tu, Yeye angeweza kuchagua jua lihubiri Injili. Angeweza kuuchagua mwezi. Angeweza kuchagua u—upepo. Lakini alimchagua mwanadamu. Na Yeye kamwe hajachagua vikundi. Watu binafsi! Unaona?

<sup>55</sup> Wala haiwezekani kuwepo na manabii wakubwa wawili duniani kwa wakati mmoja. Unaona, kila mtu yuko tofauti, ameumbwa tofauti. Kama Mungu angeweza kumpata mtu mmoja, huyo ndiye tu Yeye anayehitaji kumpata, moja kwa moja



mkononi Mwake, Yeye anaweza kufanya anayotaka. Inabidi tu apate mmoja. Katika siku za Nuhu; siku za Eliya; siku za Musa.

<sup>56</sup> Wengi waliinuka, wakati wa Musa. Unajua jinsi walivyofanya, na walitaka kusema, “Vema, wewe siye aliyemtakatifu pekee katika kundi hilo,” na—na Dathani na—na Kora.

<sup>57</sup> Na Mungu akasema, “Hebu Jitenge tu. Nitaifungua tu ardhi na kuwameza.” Unaona? Na—na kwa hiyo. . .

<sup>58</sup> Na ndipo watu wakaanza kulalamika. Akasema, “Nitaninii tu—nitaondolea mbali kitu hicho chote.”

<sup>59</sup> Na ndipo Musa hapo akachukua mahali pa Kristo, basi, kujitupa katika pengo, na kusema, “Usifanye hivyo, Bwana.” Unaona? Na, bila shaka, yeye. . . Baada ya Yeye kumchagua Musa kufanya jambo hili, Yeye hakumjilia Musa, sababu alikuwa akipachukua mahali pa Kristo wakati huo. Ilikuwa ni Kristo ndani ya Musa. Kweli kabisa.

<sup>60</sup> Sasa, tuna furaha sana siku hizi ya kwamba Mungu anajifunua kwetu. Nami ninaamini ya kwamba ile Siku iliyo kuu ndiyo kwanza inaanza kupambazuka, kuchomoza. Vimulimuli vinaanza kumemetesha. Ndege wa paradiso wameanza kuimba katika moyo wa watakatifu. Wao wanajua hilo haliko mbali sasa. Jambo fulani litatukia, halina budi kutukia tu. Kwa hiyo kama “Yeye hatendi lo lote. . .”

<sup>61</sup> Sasa, Maandiko yote yana pumzi ya Mungu. Maandiko hayana budi kuwa ni Kweli tupu kabisa. Hakuna njia ya kuliepuka hilo. Hapo ndipo sikubaliani na rafiki zetu, kanisa Katoliki. Ninaamini ya kwamba hayakuandikwa na watu wa kawaida tu. Ninaamini waliongozwa na Roho Mtakatifu. Na mambo haya yote madogo ambayo yameongezwa, wamejaribu kuongezea juu Yake; je! umepata kuona, katika kule kutatuliwa, yote yalitupiliwa mbali.

<sup>62</sup> Na Maandiko haya halisi, ya kweli, yanaingiana vizuri sana, moja kwa lingine, mpaka ha—hayahitilafiani ndani yake, hakuna. Nionyeshe kitabu kimoja ambacho kinaweza—ambacho kinaweza kuandika kifungu kimoja, angalao, bila ya kujipinga chenyewe, ama kuandika—kuandika aya moja, ama mbili. Na Biblia haijipingi Yenyewe, mahali po pote. Nimesoma ambapo wale wakinzani wa kale wakisema hivyo, lakini nimemsai kwa muda mrefu, anionyeshe ni mahali gani. Hakuna mahali hapo humu. Ni kwa sababu tu akili ya mwanadamu imechanganyikiwa. Mungu hachanganyikiwi. Yeye anajua analofanya. Anajua.

<sup>63</sup> Angalia, kama Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa, kama lisemavyo kanisa Katoliki, vema, basi kanisa hilo ni lipi? Angalieni tu makanisa tuliyo nayo. Tuna mia tisa na kitu, madhehebu mbalimbali ya makanisa. Sasa vipi. . . Moja linafundisha *hivi*, na lingine *vile*. Ni mchafuko wa jinsi gani,

basi, mtu ye yote anafanya tu lo lote wanalotaka kufanya, mnaendelea hata hivyo. Mungu hana budi kuwa na kipimo fulani, na hicho ni Neno Lake.

<sup>64</sup> Nikinena. . . Si kuwadharau Wakatoliki, sasa, maana Wa—Waprotestanti wako makosani vivyo hivyo. Lakini nilipokuwa nikizungumza na kasisi fulani, alisema, “Bw. Branham,” akasema, “Mungu yuko katika kanisa Lake.”

<sup>65</sup> Nikasema, “Bwana, Mungu yuko katika Neno Lake. Naye ni Neno.” Naam, bwana.

Akasema, “Vema, Yeye yuko katika. . . Kanisa haliwezi kukosea.”

<sup>66</sup> Nikasema, “Yeye hasemi hivyo. Lakini amesema Neno haliwezi kukosea.”

<sup>67</sup> Akasema, “Vema, tulikuwa tunafundisha ubatizo huo namna hiyo, na kadhalika.”

Nikasema, “Lini?”

Kasema, “Huko nyuma katika siku za mwanzoni.”

Nikasema, “Je! unakubali hilo kuwa ni kanisa Katoliki?”

Akasema, “Naam.”

<sup>68</sup> Nikasema, “Basi, mimi ni Mkatoliki, Mkatoliki wa mtindo wa kale. Ninaamini ile njia ya mtindo wa kale. Ninyi watu siku hizi mmelivuruga kabisa, wala ni vigumu kupata cho chote mnachofundisha kutoka katika Maandiko. Kuombewa na wanawake pamoja na wafu, na mambo haya mengine yote, na, loo! jamani, hakuna-cha-kula-nyama, na, loo! sijui nini tena, unaona.” Nikasema, “Nionyeshe hayo katika Maandiko.”

<sup>69</sup> Akasema, “Si lazima yawemo humo. Mradi tu kanisa linasema hivyo, ndio hivyo hivyo. Haijalishi hayo yaseme nini, kanisa ndilo lenye sauti.”

<sup>70</sup> Nikasema, “Biblia ilisema, ya kwamba, ‘Mtu ye yote atakayeongeza neno moja Kwake, ama kuondoa Moja, ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima.’ Kwa hiyo, ni Neno! Ninaamini Neno.”

<sup>71</sup> Sasa, na, basi, kama Amosi ikisema, na Maandiko mengine yanayoambatana nayo, ya kwamba kama. . .

<sup>72</sup> Nanyi mnakumbuka, juu ya jambo hili, tunagusia tu mambo Yake muhimu. Ninii tu, jamani, kama. . . Ninapoingia kwenye chumba kile pale, na—na ule Upako unakuja, kama ningaliweza kuandika yale ambayo Yeye. . . yale yote yanayoendelea, ningekaa hapa kwa miezi mitatu kwenye mmoja wa Mihuri hii. Kwa hiyo ninagusia tu sehemu-sehemu na kuliacha, yale tu yanayoonekana kana kwamba hayawezi kuwasonga watu roho. Lakini, hata hivyo, si sana kuwaudhi, bali ili kwamba tu, nikiamini, linge—linge koleza kitu hicho. Mnajua ninalomaanisha.

<sup>73</sup> Sasa, angalia hili sasa, kama “Mungu hafanyi lo lote,” alisema Amosi, “mpaka kwanza awafunulie watumishi Wake manabii.” Na, halafu, tunaona yale Yeye anayofanya. Lazima iwe kwamba Yeye anajitayarisha kufanya jambo fulani, yale Yeye anayoyafunua sasa. Mungu yuko karibu kuja jukwaani, katika hukumu, ninaamini. Yuko karibu kufanya jambo fulani. Na jambo moja tena, linashuhudia kweli, tuko katika siku za mwisho. Tuko katika mwisho wa wakati, Wakati wa Kanisa la Laodikia sasa, kwa kuwa mambo haya yalikuwa yafunuliwe tu kwenye siku ya mwisho.

<sup>74</sup> Sasa, hebu wazia tu jambo hilo sasa. Hebu tuninii tu—tujaribu kuyaingiza yale tunayoamini kwamba Roho Mtakatifu angetutaka tujue.

<sup>75</sup> Sasa kumbukeni, “Hakuna lo lote linaloweza kufunuliwa; Mungu hatafanya neno lo lote, hata kidogo, mpaka kwanza alifunue kwa watumishi Wake, manabii.” Na kabla ya Yeye hajafanya neno lo lote, hulifunua. Na hapo anapolifunua, unaweza kukumbuka jambo hili, jambo fulani liko njiani. Unaona, linafunuliwa.

<sup>76</sup> Na mambo haya tunayozungumza juu yake yalikuwa yafunuliwe katika siku ya mwisho, kabla tu ya ile Baragumu ya mwisho, katika mwisho wa Ujumbe wa wakati wa mwisho wa kanisa. Hiyo ni kweli. Kama unataka kusoma jambo hilo sasa, unaweza kufungua. . . Wewe, niliwarejesha wakati huu huu, jana usiku, mara tatu, Ufunuo 10:1-7, unaona. “Na katika siku za kupiga baragumu ya Ujumbe wa malaika wa saba, siri ya Mungu itafunuliwa na kumalizika.” Na kuna jambo moja tu lililosalia. Wakati Kitabu hiki chenye muhuri saba kitakapokwisha kufunguliwa, basi siri yote ya Mungu. . .

<sup>77</sup> Mbona, tumeiingilia kuichunguza Hiyo, kwa miaka mingi. Na kulingana na Maandiko, basi, sisi. . . Hapakuwapo na njia ya kuifahamu mpaka siku ya leo, kwa sababu ilikuwa imefichwa. Tumeona mfano wake, jinsi lilivyoonyeshwa kwa mfano, bali haingeweza kufunuliwa kwa usahihi mpaka siku ya mwisho. Unaona? Sasa, basi, hatuna budi kuwa hapo, kwenye—kwenye wakati wa mwisho.

<sup>78</sup> Sasa, kumbukeni. Msi- . . . Na msisahau sasa, ya kwamba, “Yeye hafanyi lo lote mpaka awafunulie.” Wala msisahau, pia, ya kwamba Yeye hufanya jambo hilo katika njia iliyo rahisi, hivi kwamba, “Wenye elimu na wenye maarifa wanalikosa.” Sasa, kama mkitaka kuandika jambo hilo, hilo ni Mathayo 11:25-26. Pia, kumbukeni. “Yeye hafanyi neno lo lote mpaka awafunulie.” Naye hulifunua kwa jinsi ambavyo kwamba watu wenye akili, wenye elimu linawapita. Kumbukeni, kitu ulimwengu ulichotamani ilikuwa ni maarifa badala ya Neno, wakati dhambi ya kwanza ilipofanya ilichofanya. Msisahau jambo hilo sasa.

Loo! jinsi tunavyopaswa kuwa watu wenye shukrani, kuwazia jambo hilo!

<sup>79</sup> Sasa angalieni tu mambo yanayotendeka! Angalieni mambo ambayo Yeye ametwambia! Angalieni hapa maskanini, ninyi watu ambao tulikulia hapa. Sasa nitawaomba wanaorekodi ninii. . . Vema, endeleeni, yanaseni. Lakini, angalieni, nitasema tu jambo hili kwa watu wa hapa maskanini, ninyi ambao mmekuwa hapa. Ninamwagiza ye yote wenu, katika Jina la Bwana Yesu, kunyoshea kidole chako jambo mojawapo, kati ya mamia ya mambo ambayo yamesemwa kabla hayajatimia, na msememe hayakutimia. Niambienu wakati mmoja, ya kwamba hapa jukwaani, huko nje, po pote pale ilipokuwa, ambapo Yeye aliwahi kunena jambo lo lote ambalo halikutimia vivyo hivyo kikamilifu kabisa. Vipi? Je! Mawazo ya mwanadamu yangeweza kuwa namna hiyo? Hasha.

<sup>80</sup> Wakati Yeye alipotokea kule chini mtoni, miaka thelathini na mitatu iliyopita ifikapo Juni hii ijayo, katika namna ya Nuru! Ninyi watu wa zamani mnakumbuka ya kwamba niliwaambia, tangu nilipokuwa mvulana mdogo, Sauti ile na Nuru ile. Na watu walidhania, kidogo nimerukwa na akili. Bila shaka, labda ningaliwazia jambo lile lile, kama ni mtu fulani amesema jambo hilo. Lakini sasa haiwapasi kushangazwa Nalo sasa. Na Kanisa halijashangaa tangu mwaka wa 1933, kule chini mtoni siku ile, ambako nilikuwa nikibatiza mamia ya watu!

<sup>81</sup> Ninakumbuka yule mvulana wa Marra alichoniambia, alisema, “Unaenda kuwatumbukiza hao watu, Billy?” Maskini Jim Marra hapa chini, nafikiri amekufa sasa. Nafikiri aliuwawa mahali fulani huko; mwanamke fulani alimpiga risasi. Lakini yeye—yeye aliniuliza, “Unaenda zako kuwatumbukiza watu hao majini?”

<sup>82</sup> Nikasema, “La, bwana. Ninaenda kuwabatiza katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo.”

<sup>83</sup> Na kulikuwa na mwanamke aliyekuwa akienda pamoja na kundi hilo. Akamwambia mwanamke mwingine, akasema. . . akatoa tamshi, kitu fulani juu ya jambo hilo. Akasema, “Vema, nisingejali kutumbukizwa.” Kasema, “Hilo ni sawa. Sijali mimi.”

<sup>84</sup> Nikasema, “Rudi na ukatubu. Hustahili kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo.” Unaona?

<sup>85</sup> Hili si jambo la kuchezea. Ni Injili ya Kristo, iliyofunuliwa kwa agizo, Neno. Ninii tu, sasa, kama unasema, “Upuuzi na ujinga,” ungeliveza kuliweka mahali pengine. Lakini, kumbuka, imeahidiwa katika Neno ya kwamba jambo hili lingetukia, na vile vile hasa ingelikuwa. Na ndilo hili hapa.

<sup>86</sup> Ndipo, chini kule siku hiyo, wakati walipokuwa wamesimama kando ya mto! Na Malaika wa Bwana, ambaye niliwaambia ya kwamba ilionekana kama nyo—nyota ama kitu

fulani kwa mbali, kisha akakaribia, na nikawaambia jinsi ile Nuru ya zumaradi ilivyoonekana. Na ikawa Hiyo hapo inakuja, moja kwa moja hapo mtoni nilipokuwa nikibatiza.

<sup>87</sup> Ambapo, wafanya biashara hapa jijini, walisema, “Hiyo ilikuwa na maana gani?”

<sup>88</sup> Nikasema, “Hiyo haikuwa ni kwa ajili yangu. Hiyo ilikuwa ni kwa ajili yenu. Mimi ninaamini. Unaona? Hiyo ilikuwa ni kwa ajili yenu, kwamba Mungu alifanya jambo hilo, kuwajulisha ya kwamba ninawaambia yaliyo Kweli.” Kwa vile nilikuwa ninaonekana ni mtoto, kivulana, na nikiwa na umri wa miaka kama ishirini na mmoja, wao—wao hawangeweza kuamini jambo hilo, unaona, kwa sababu ni jambo la kiwango cha juu sana kwa mtoto mdogo. Halafu nilikuwa nikifikiria . . .

<sup>89</sup> Ndugu Roberson hapa, mmoja wa wadhamini wetu, nilimwona hapa dakika chache zilizopita. Alikuwa akiniambia juzijuzi kuhusu tulipokuwa Houston wakati ile picha pale ilipopigwa, mnayoiona. Nami nilikuwa . . . Kwenye yale mahojiano, nilikuwa nimeanza kusema jambo fulani kuhusu hiyo, juzijuzi usiku. Ndugu Roy alikuwa ndiye pekee . . . pamoja na mtu mmoja mwingine zaidi, alikuwa ndiye mtu pekee katika kundi aliyekuwa na kinasasauti. Kilikuwa ni kimoja cha vile vinasasauti vya kale vya waya. Ninamwona Ndugu Roberson sasa, pamoja na mkewe. Kwa hiyo, na—na huyu, Bibi Roberson alikuwa mgonjwa.

<sup>90</sup> Ndugu Roy alikuwa askari mzoefu wa vita wa siku nyingi. Na miguu yake alilipuliwa, nao wakamweka sehemu fulani huko afe. Yeye alikuwa afisa katika—katika Jeshi. Na bunduki ya Kijerumani ya nane-nane ilikipiga kifaru hiki ambamo alikuwa, na karibu imuue mtu huyo, na kumpasua vipande-vipande. Wakamtoa nje, afie huko, kwa muda mrefu. Nao walisema hangeweza kutembea hata kidogo, kwa sababu miguu yote miwili ilikuwa imekatwa, mishipa yake ya fahamu, na kadhalika. Jamani, yeye karibu anaweza kunishinda katika kutembea.

<sup>91</sup> Lakini ilikuwa ni kitu gani? Kulikuwa na kitu fulani alichona, ndipo akaenda Houston. Naye alikuwa akiniambia juu ya mkewe. Na Ndugu Roberson ana—ana waya; utauunganisha kwenye kinasasauti. Na baada ya ibada hapa kwisha, vema, atawafungulieni nyote hiyo kanda, natumaini. Na kwenye kile kinasasauti cha kale cha waya pale, amenasa ibada zangu zilizofanyika Houston. Na halafu basi mkewe, yeye alisema, anazo pale, wala yeye hakutambua jambo hilo mpaka hivi majuzi.

<sup>92</sup> Mama huyo alikuwa, loo! alikuwa na huzuni sana. Alikuwa mgonjwa, naye alitaka kuingia kwenye mstari wa maombi. Wao hawakunjua mimi hata kidogo, nami sijawahi kuwaona maishani mwangu. Kwa hiyo alikuwa amesimama karibu na

di—dirisha siku hiyo, akiangalia nje, akiwa na moyo mzito sana, unajua, na amefadhaika, na akitamani sana apate kadi ya maombi, ili aingie mstarini.

<sup>93</sup> Na, ilitukia kwamba, usiku huo akaingia kwenye mstarini wa maombi, ama usiku uliofuata, ama kitu kama hicho. Ninaamini, usiku uo huo. Ndipo akaingia mstarini. Na wakati alipokuja jukwaani, Roho Mtakatifu akamwambia, akasema, “Sasa, wewe hutoki hapa. Umetoka katika mji unaoitwa New Albany.” Kisha akasema, “Ulikuwa umeketi karibu na dirisha leo, ukiangalia nje, huku umefadhaika sana kuhusu kupata kadi ya maombi.” Hayo hapo, kwenye kanda, miaka mingi iliyopita.

<sup>94</sup> Na ndipo wakati mkutano ulipokuwa unaanza, wakati Roho Mtakatifu alipokuwa pale. . .Huo ulikuwa ndio mkutano wa kwanza. Tulikuwa tu na watu kama elfu tatu, ndipo tukafikia kwenye elfu nane, halafu ikaendelea ikafika kwenye kama elfu thelathini. Kwa hiyo basi katika ninii. . . Nilipokuwa nikizungumza kwenye ninii. . . Mmoja wa mikutano ya kwanza kabisa, nikasema, “Sijui ni kwa nini ninasema jambo hili.” Sasa, yako kwenye kanda. “Lakini, ni, tuna- . . .Huu utakuwa mmoja wa nyakati zilizo muhimu sana maishani mwangu. Jambo fulani litatukia katika mkutano huu, ambalo litakuwa kubwa sana kuliko lile ambalo mtu ye yote ameshawahi kuona huko nyuma.”

<sup>95</sup> Na ilikuwa tu yapata siku nane ama tisa, siku kumi baada ya jambo hilo, wakati Malaika wa Bwana alipotokea mbele ya watu kama elfu thelathini, na akashuka, na picha ikapigwa. Ndiyo ile iliyoko kule, sasa hivi, ambayo imehaki-milikishwa huko Washington, D.C., kama Kiumbe chenye uhai pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha ulimunguni.

<sup>96</sup> Ndipo nilizungumzia juu ya, mwajua, kusema ya kwamba wakati mwingine, chini ya upambanuzi, nasema, “Mtu fulani ametiwa uvuli wa mauti. Kuna kifuniko cheusi, cha uvuli. Watu fulani wanakaribia kufa.”

<sup>97</sup> Halafu hapa katika Pines ya Mashariki, ama Pines ya Kusini, ninaamini ndiyo huko, wakati nilipokuwa tu kule kwenye mkutano wa mwisho. Mama mmoja msichana ameketi pale, na kitu Fulani kikamwambia, “Piga picha ya jambo hilo, upesi sana,” wakati nilipokuwa nikizungumza na mama mmoja. Na hapo ikatokea. Nafikiri itakuwa kwenye ubao wa matangazo; imekuwa hapo, kwa muda kidogo wa kutosha. Kuna hicho kivuli cheusi kinachoning’inia juu ya bibi huyo.

<sup>98</sup> Mwanamke huyo akapiga picha nyingine, mara tu Roho Mtakatifu alipotangaza jambo hilo. Kilikuwa kimeondoka. Kasema, “Utapona. Bwana amekuponya. Kansa imeondoka.” Na basi hivyo ndivyo iliyokuwa. Naye aliponywa. Unaona? Haya basi. Unaona?

<sup>99</sup> Inaonyesha tu ya kwamba Mungu anajua ni saa ngapi ya mchana. Sisi hatujui. Inatupasa tu kumtii.

<sup>100</sup> Sasa tunaweza kuendelea tu kuzungumza, lakini hebu na twende chini hapa sasa, kwa dakika moja tu, na tuguse Mhuhuri huu wa nyuma, ili kwamba tuweze kuunganisha huu pamoja Nao. Sasa, ni marudio tu, kwa muda mcha-...muda kidogo, ule—ule mwingine, Muhuri wa Kwanza.

<sup>101</sup> Tunaona, katika kule kuvunjwa kwa Muhuri wa Kwanza, Shetani ana m-mtu maalum, mtu wa dini. Je! umewahi kumchunguza huyo mpanda farasi mweupe? Ambaye, wao, ilikuwa ikidhaniwa ya kwamba huyo alikuwa...lile Kanisa la mwanzoni likipiga hatua; lakini, loo, jamani, jambo hilo limefundishwa katika miaka mingi iliyopita, lakini lisingeweza kuwa hivyo. Angalia tu wakati hiyo mingine, wakati tutakapofungamanisha hiyo mingine pamoja, ndipo ulione lilivyo, unaona. Sasa, wala sijui vile hiyo mingine itakavyokuwa, bado. Lakini ninajua haina budi ije iingie na kupatana vizuri kabisa, kwa maana ni Kweli. Ni kweli. Hiyo ni serikali ya kidini ya Roma, hasa.

<sup>102</sup> Hawa watu wanaodhani kwamba Wayahudi ndio mpinga-Kristo, kwa kweli wameenda nje ya mtari kwa maili milioni moja. Kamwe usifikiri ya kwamba Wayahudi ndio mpinga-Kristo. Macho yao yalipofushwa, makusudi, ili kwamba tupate njia ya kuingia, ikitupa sisi wakati wa kutubu.

<sup>103</sup> Lakini mpinga-Kristo ni Mmataifa. Kweli kabisa. Ni mtu fulani mwigizaji wa Kweli; *mpinga*, “dhidi.” Sasa, huyu mtu maalum sana, loo, jinsi alivyofanyika mtu mkuu, na—na hatimaye akatawazwa. Na halafu, baada ya kutawazwa, akavikwa taji. Na sasa, yeye, baada ya hayo, aliabudiwa badala ya Mungu.

<sup>104</sup> Sasa, angalia, kabla ya jambo hilo kupata kutukia. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Huyo alikuwa ni nani? Ni Kitu gani kilichokuwa juu ya Paulo, katika Wathesalonike 2:3, kilichosema mtu huyo angekuja? Kwa nini mtu huyo akaangalia kupitia katika wakati mzima na kuona jambo hilo? Yeye alikuwa ni nabii wa Mungu. Hakika. Kwa nini ilikuwa... .

<sup>105</sup> Alisema, “Roho anena waziwazi, ya kwamba nyakati za mwisho watu watajitenga na imani, nao wangesikiliza nini zidanganyazo...” Unajua *kudanganya* ni nini. Roho idanganyayo kanisani, yaani mkasisi. “Roho zidanganyazo, za makasisi, matendo ya mashetani; unafiki kanisani.”

<sup>106</sup> “Wakaidi, wenye kujivuna,” elimu, unaona, werevu, wenye akili; “wenye mfano wa utauwa.” (Wanaenda tu, wanasema, “Vema, sisi ni Wakristo; yatupasa kwenda kanisani.”) “Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana mafunuo, Nguvu za kutenda kazi kwa Roho; hao nao ujiepushe nao.” Unaona? Sasa angalia, yeye alisema, “Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu, na watawachukua mateka wanawake wajinga...” Hiyo haimaanishi wanawake wenye

Roho Mtakatifu. “Wanawake wajinga waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi.”

107 Tamaa za namna nyingi! Wao wanapenda tu kuingia katika kila kitu kidogo wanachoweza kuingia ndani yake, na kila namna ya mashirika; na kuishi vyo vyote wapendavyo, na, bado, “Tunaenda kanisani. Sisi ni watu wazuri tu kama mtu ye yote yule.” Madansi, karamu, kukata nywele zao, kujipodoa, kuvaa cho chote watakacho; hata hivyo, “Si—sisi ni Wapentekoste. Sisi—sisi ni wazuri tu kama mtu mwingine ye yote.” Loo! Kazi zako mwenyewe zinakutambulisha. Angalia.

108 Lakini alisema, “Watu walioharibika akili zao, kuhusu ile Kweli.” Kweli ni nini? Neno, ambalo ni Kristo. “Kuhusu ile Kweli.”

109 “Loo, unafanya . . . Wewe, wewe ni mkandamiza wanawake. Wewe ni mchukia—wanawake. Wewe unafanya *hili, lile*.”

110 La, bwana. Hiyo si kweli. Huo ni u—uongo. Mimi siwachukii wanawake. La, bwana. Wao ni dada zangu, kama wao ni dada. Lakini jambo ninaloninii . . .

111 Upendo husahihisha. Kama hausahihishi, si upendo. Kama husahihisha, basi, kama ni upendo, ni—ni upendo wa fileo wala si wa agape, kweli nitakwambia. Wao wanaweza kuwa na upendo kidogo wa fileo kwa ajili ya mama fulani mwenye sura nzuri. Lakini upendo wa agape ni jambo lingine, huo ni upendo unaonyosha jambo hilo, na kukutana na Mungu huko mahali fulani tunakoweza kuishi Milele. Unaona? Mimi sikumaanisha jambo hilo, labda, kwa jinsi vile lilivyosikika, lakini ninaninii . . . Mnajua yale ni—ni . . . ninatumaini mnafahamu. Vema.

112 Sasa, lakini, kumbukeni, alisema, “Kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Musa, vivyo hivyo na hawa watapingana. Lakini upumbavu wao ulidhihirika mara moja.”

113 Kwa nini? Wakati Musa alipoagizwa kufanya jambo fulani lililoonekana ni la kimapinduzi sana, lakini, alishuka akaenda kule mwaminifu tu kama alivyoweza kuwa. Ndipo Mungu akamwambia achukue hii, fimbo hii, na kuitupa chini, na ingeuka iwe nyoka. Ndipo, Yeye akafanya jambo hilo, kumwonyesha jambo ambalo lingetukia. Na mbele ya Farao, alisimama pale kama vile tu Mungu alivyokuwa amemwagiza, na akatupa chini ile fimbo yake, ndipo ikageuka kuwa nyoka.

114 Na hapana shaka, Farao alisema, “Hila rahisi ya kichawi!” Ndipo anaondoka kwenda na kuwaleta Yane na Yambre wake. Kasema, “Tunaweza kufanya mambo hayo, sisi pia.” Ndipo akatupa ile fimbo chini, nazo zikawa nyoka.

Sasa Musa angefanya nini?



115 Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni kuonyesha ya kwamba, kila kitu halisi cha Mungu, Ibilisi ana igizo lake. Wao wanaiga, ili kuwaondosha watu njiani.

116 Musa alifanya nini, ati aseme, “Vema, nadhani nilifanya kosa. Afadhali nirudi?” Yeye alisimama kimya tu, kwa kuwa alikuwa ametekeleza agizo lake, kikamilifu.

117 Halafu, muda si muda unajua, nyoka wa Musa akamla yule mwingine. Unaona? Uliwahi kuwazia kilichompata huyo nyoka mwingine? Alienda wapi? Musa aliitwaa ile fimbo akaondoka na akaenda nayo. Alifanya miujiza nayo. Na huyo nyoka alikuwa ndani ya fimbo hii nyingine. Unaona? Hiyo ni ajabu. Sivyo? Naam, bwana.

118 Sasa, mpinga-Kristo anaonekana waziwazi, kidogo kidogo. Nataka mwone jambo hili. Sasa, mnaposikia . . .

119 Sasa, kwa marafiki wangu Wakatoliki, hebu ketini tu kimya kwa dakika moja, na sasa; na ndipo tutaona ambapo Waprotestanti; mahali tulipo sisi sote, unaona.

120 Angalia, lile kanisa la kwanza, wakati kanisa Katoliki linaposema ya kwamba wao walikuwa ndio wa kwanza, kanisa la awali, wao wanasema kweli kabisa. Walikuwa wa kwanza. Walianzia Pentekoste. Hapo ndipo kanisa Katoliki lilipoanzia. Sasa, wakati mmoja ilikuwa ni vigumu kwangu kuamini jambo hilo, mpaka niliposoma historia, nami nikaona kwamba ilikuwa ni kweli. Walianzia Pentekoste. Lakini walianza kuondoka mahali walipokuwa, nanyi unaona mahali walipo.

121 Na kama Wapentekoste wakiondoka mahali walipo kwa kasi wanayoondoka nayo sasa, haitahitaji kwenda miaka elfu mbili. Katika miaka mia moja tangu sasa, watakuwa mbali sana kuliko kanisa Katoliki lilivyo. Hiyo ni kweli.

122 Lakini hebu angalia, jinsi, huyu mpanda farasi mweupe. Sasa hebu tuliwekee msingi jambo hili, kidogo, mpaka tutakapoufikia Muhuri huu. Sasa angalia mpanda farasi mweupe, wakati alipotoka, yeye—yeye anatumika katika hatua tatu. Ibilisi, kama nilivyowathibitishia usiku wa juzi, yuko katika utatu, kama tu Mungu alivyo. Lakini ni Ibilisi yeye yule wakati wote, katika hatua tatu. Angalia hatua zake. Katika hatua ya kwanza, yeye aliingia . . .

123 Roho Mtakatifu alishuka, na watu walikuwa na kila kitu shirika. Na Roho wa Mungu alikuwa juu yao. Na mitume wakaenda nyumba kwa nyumba, wakimega mkate pamoja na watu. Na kulikuwako na ishara kubwa na maajabu yaliyofanywa.

124 Na—na halafu, muda si muda unajua, Shetani alianza kusababisha kutokee manung'uniko.

125 Basi, baada ya kitambo kidogo, hawa watumwa na maskini wa nchi, waliompokea Roho Mtakatifu, walienda mahali mbalimbali, wakishuhudia. Wakawashuhudia bwana zao.

126 Na muda si muda, kukaanza kuja, loo, kama vile makapiteni wa jeshi na—na watu mbalimbali. Waheshimiwa wakaanza kuona ushujaa, na miujiza na ishara ambazo watu hawa walifanya, kwa hiyo wakakubali Ukristo.

127 Vema, basi, unaona, wakati alipoukubali Ukristo, na wakaenda kule mahali wanapokutana, katika ukumbi mdogo uliochakaa, wenye giza, mchafu; na huku wakipiga makofi, na kupiga makelele, na kunena kwa lugha, na kupata jumbe. Mbona, yeye hangezwa kabisa kupeleka mambo hayo kwa mshirika mwe—mwenzake, ama ye yote yule, katika biashara yake. “Yeye hangeamini jambo Hilo kamwe, vile ilivyokuwa.” Hasha. Kwa hiyo, hana budi kulipamba. Kwa hiyo wakaanza kukutana, na wakaanza kufikiria, “Sasa tutatengeneza kitu fulani tofauti kidogo.”

128 Naye Yesu, mara tu pale pale, kwenye wakati wa kwanza wa kanisa, Yeye aliwaambia. Katika sura ya 2 ya Ufunuo hapa, “Nina neno moja juu yenu, kwa sababu ya matendo haya ya Wanikolai.”

129 *Nikao*, “kushinda” wafuasi. Kwa maneno mengine, wanataka kufanya, badala ya kila mtu kuwa ndiye yeye, wao wanataka kumfanya mtu fulani mtakatifu. Walitaka kufanya namna fulani ya . . . Walitaka kulifananisha na upagani, kule walikotoka, nao hatimaye wakafanya jambo hilo.

130 Sasa angalia. Kwanza, “Unikolai.” *Unikolai* uliitwa, katika Biblia, “upinga-Kristo,” kwa maana ulikuwa ni kinyume cha Fundisho la asili la Kristo na mitume.

131 Sitaki kutaja jina la mtu huyu. Yeye ni mtu mashuhuri. Lakini nilikuwapo kwenye mkutano wake, hapa miaka michache iliyopita. Naye alijua nilikuwa niko hapo, kwa maana nilikuwa nimempa mkono. Naye alisema, “Loo, unajua, tuna wale siku hizi wanaowaita Wapentekoste.” Naye akasema, “Wao, wao wanategemea Kitabu cha Matendo.” Basi akasema, “Unaona, Matendo ilikuwa ni fremu tu ya Kanisa.”

132 Ungeweza kuwazia, mtu ambaye amekwisha kuisoma Biblia, mzee hodari, na amesoma Biblia jinsi mtu huyo alivyofanya, halafu angetoa tamshi kama hilo? Lilisikika, halininii. . . Hata ha—halisikiki kama ni Roho Mtakatifu. Vema, haipaswi kuwa ni fremu, po pote pale.

133 Kwa sababu, mtu ye yote aliye na ufahamu wa kawaida angejua ya kwamba Matendo ya Mitume hakikuwa ni matendo ya mitume. Kilikuwa ni matendo ya Roho Mtakatifu ndani ya mitume. Hivi hamjui jinsi tulivyolinganisha jambo hilo kwenye nyakati za kanisa? Hao Wenye Uhai wakiketi pale, wakililinda lile Sanduku la Agano pale. Mathayo, Marko, Luka,

na Yohana, wamesimama pale, Wakilinda Hilo. Na ndani Mle ndivyo ilivyotendeka, kama matokeo ya maandishi ya Mathayo, Marko, Luka, na Yohana.

134 Hicho ndicho ule mti ulichochipusha, tawi lake la kwanza, na hivyo ndivyo ilivyotendeka. Na kama mti huo ukipata kuchipusha tawi lingine, wao wataandika Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake. Maana, unaona, Uhai ule ule hauna budi kuwa katika jambo lile lile.

135 Kwa hiyo sasa, siku hizi, tunapoangalia kwenye makanisa yetu ya kimadhehebu, ya Kimethodisti, ya Kibatisti, ya Kipresbiteri, ya Kiluteri, kanisa la Kristo (linavyoitwa), na Wapentekoste na kadhalika, tunaona wapi jambo hilo? Hulioni.

136 Nitakubali ya kwamba Wapentekoste ndio walio na jambo lililo karibu sana Nalo, waliopo, kwa maana wao wako hapa juu katika Wakati wa Kanisa la Laodikia. Wao walikuwa na Kweli na wakaikataa. Wakawa vuguvugu Nayo, ndipo Mungu akawatapika kutoka katika kinywa Chake. Hiyo ni kulingana na Maandiko kabisa.

137 Huwezi kuyafanya hayo Maandiko yaseme uongo. Unaona? Yatakuwa ya kweli, daima. Usijaribu kuninii. . . Jambo pekee, usijaribu kupatanisha mawazo yako kwenye. . . ama Maandiko kwenye wazo lako. Lakini jipatanishe wewe mwenyewe na Maandiko. Hivyo ndivyo, basi unvyoambatana na Mungu. Haidhuru itakubidi kupunguza kiasi gani, ama kuweka kando, jipatanishe na Hilo. Unaona?

138 Angalia kile alichofanya wakati aliposhuka mara ya kwanza. Vema, kama Mungu alitenda namna hiyo mara ya kwanza, hana budi kutenda namna hiyo mara ya pili. Hana budi kutenda namna hiyo hiyo kila wakati, au alitenda vibaya mara ya kwanza.

Unaona, sisi kama wanadamu, tunaweza kukosea. Mungu hawezi.

139 Uamuzi wa kwanza wa Mungu ni mkamilifu. Na jinsi alivyochagua kufanya mambo, hakuwezi kuwa na njia nyingine, njia bora zaidi. Yeye hawezi kuifanya bora zaidi, kwa sababu ni kamilifu, kwanza. Kama si kamilifu, basi yeye si asiye na kikomo. Na kama Yeye hana kikomo, basi Yeye ni anayejua yote. Na kama anajua yote, basi Yeye ana nguvu zote. Amina! Hana budi kuwa namna hiyo, apate kuwa Mungu. Unaona? Kwa hiyo hu—huwezi kusema, sasa, “Yeye amejifunza zaidi.” Hakujifuza zaidi, Yeye ndiye ile—Yeye ndiye chemchemi yenyewe ya hekima yote. Unaona?

140 Hekima yetu hapa inatokana na Shetani. Tuliirithi kutoka Edeni, mahali tulipobadilisha imani kwa maarifa. Hawa alifanya jambo hilo.

<sup>141</sup> Sasa, kwanza yeye aliitwa mpinga-Kristo. Hatua ya pili, aliitwa nabii wa uongo, kwa maana roho huyo miongoni mwa watu alifanyika mwili.

<sup>142</sup> Mnakumbuka, yule mpanda farasi mweupe sasa hakuwa na taji wakati alipoanza, lakini baadaye yeye angeninii . . . alipewa taji. Kwa nini? Alikuwa ni roho ya Unikolai, kwanza; na baadaye akafanyika mwili katika mwanadamu; na halafu akavikwa taji, na akapokea kiti cha enzi na kuvikwa taji. Na ndipo akatumika namna hiyo kwa muda mrefu, kama tutakavyoona tunaponinii . . . Mihuri inapovunjwa.

<sup>143</sup> Na halafu tunaona, baada ya muda huo mrefu, Shetani alifukuzwa kutoka Mbinguni. Na ndipo akashuka, kulingana na Maandiko, na kujitawaza mwenyewe. Wazia tu, akajifanyia kiti cha enzi mwenyewe katika mtu huyo, ndipo akawa mnyama. Naye alikuwa na mamlaka, mamlaka kuu sana, kama vile alivyofanya, miujiza yote na kila kitu, ambayo—ambayo, ama mauaji na vita vya umwagaji damu na kila kitu ambacho—ambacho Rumi ingeweza kutunga. Vema. Aliua kwa adhabu katili, ya Kirumi. Ninii tu, loo, jinsi tungeweza kuyavunjavunja baadhi ya Maandiko hapa!

<sup>144</sup> Kumbukeni, Yesu Kristo alikufa chini ya adhabu ya Rumi, adhabu ya kifo.

<sup>145</sup> Ujumbe nilio nao moyoni mwangu, kuhubiri hapa kwenye mkutano huu mwingine ujao, kwenye Ijumaa Kuu alasiri, unakabiliana na mambo matatu, manne, unaona. “Hapo wao wakamsulibisha Yeye.” “*Hapo*,” mahali patakatifu sana, pa kidini sana ulimwenguni palikuwa ni Yerusalemu. “*Wao*,” watu (wanaodhaniwa kwamba) ndio walio watakatifu sana ulimwenguni, Wayahudi. “Hapo wao *wanamsulibisha*,” adhabu katili sana ambayo Rumi ingeweza kutoa. “Kumsulibisha Yeye. Nini? Mtu mkuu sana aliyewahi kuishi. “Hapo wao wakamsulibisha Yeye.” Loo, jamani!

<sup>146</sup> Mungu anisaidie kuitikisa kwenye lile kundi la wafanyabiashara, mpaka waweze kuona mahali wanaposimama. Vema. Sasa, si kwamba nataka nitofautiane, si kwamba nataka niudhi mtu; lakini nilitikise Hilo, mpaka hao ndugu waweze kuona ya kwamba watu wao mashuhuri na mababa watakatifu, na mambo wanayoandika kwenye gazeti hili la Wafanya biashara, ni upuzi. Wakristo hawapaswi kumwita mtu ye yote “Baba.” Wanaanza jambo hilo. Nimejaribu kuwasaidia katika kila jambo ninaloweza kufanya. Unaona sasa mahali kanda hii inakokwenda. Kwa hiyo, nimemaliza. Kweli sitahusika na uhusiano wo wote na jambo hilo. Vema. Kwanza, kumbukeni Kristo.

<sup>147</sup> Kwanza, kama Uni-. . .Unikolai, wakati wa Unikolai uliomba nini? Waliomba watoke kwenye kundi hilo la watu wanaopiga makelele na kupiga makofi, na kuonekana kama

aibu; kama walivyofanya Pentekoste, kutenda kama walevi, wakiyumbayumba katika Roho, na kadhalika. Hawakutaka upuuzi kama huo. Walisema walikuwa wamelewa. Na wakati hao watu mashuhuri... Sikilizeni! Msikose jambo hili. Linaweza kusikika la kiwazimu kwenu, lakini ni Kweli. Wakati watu ma—mashuhuri walipoanza kuingia, hawangeweza kulikubali jambo hilo.

<sup>148</sup> Kile kinachomfanya Mungu kuwa mkubwa, ni kwa sababu yeye ni mkubwa kutosha kujidhili. Hicho ndicho kinachomfanya kuwa mkubwa. Hakuna kilicho kikubwa kumzidi. Naye alijishusha chini sana ambavyo mtu ye yote asingeweza kushuka, mwanadamu ye yote aliwahi kushuka. Yeye alikuwa Mfalme wa Mbinguni, naye akaja kwenye—kwenye mji ulio mdogo sana duniani, Yeriko. Naye akashuka chini sana hata mtu aliye mfupi sana mjini alimpasa kuangalia chini, apate kumwona Yeye. Hiyo ni kweli? Zakayo. Hiyo ni kweli. Aliitwa jina baya kuliko yote mwanadamu ye yote anaweza kuitwa, “mchawi, pepo, Beelizebuli.” Hivyo ndivyo ulimwengu ulivyomdhanania. Alikufa kifo cha kikatili kupita vyote. Hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Alitupwa nje, na kila madhehebu.

<sup>149</sup> Lakini wakati Mungu alipomwinua, juu sana hata inambidi kuangalia chini apate kuona Mbinguni. Unaona jinsi, Mungu, katika unyenyekevu. Unaona? Naye akampa Jina lililo kuu sana hata jamaa yote ya Mbinguni inaitwa kwa Jina Lake, na kila jamaa ya du—duniani. Jamaa yote ya duniani inaitwa “Yesu.” Jamaa zote za Mbinguni zinaitwa “Yesu.” Na Jina kuu sana, hivi kwamba, kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri, kwake kuwa Yeye ni Bwana; aidha hapa ama kuzimu. Kuzimu kutalipigia goti. Kila kitu kingine chote kitaliinamia. Unaona? Lakini kwanza ilikuwa ni unyenyekevu, ndipo likawa kuu. Unaona? Acha Mungu atukuze. “Yeye ajidhiliye, Mungu atamkweza.” Unaona?

<sup>150</sup> Sasa, tunaona hii roho ya *nikao* ilitaka maarifa, ina akili zaidi. Ilibidi ilijadili, kama ilivyokuwa katika Edeni, kujadili dhidi ya Neno la Mungu, kwa hekima, nalo kanisa likashawishika kwa jambo hilo. Ilikuwa ni nini?

<sup>151</sup> Sasa, hebu na tuseme, tulichukue kanisa hili hapa, na tuchukue kundi la watu kama tulivyo sisi, kama hukuwa umejazwa kabisa Roho. Na hebu na tuchukue, tuseme... Sasa, sina kitu dhidi ya meya wa mji wetu. Sidhani kama ninamjua, Bw. Bottorff. Je! yeye angali ni meya, Bw. Bottorff? Unaona, sininii. . . Bw. Bottorff ni rafiki wangu mzuri, unaona. Lakini, tuseme, meya wa mji, na jeshi lote la polisi, na—na majemadari wote, nao—nao wote waje hapa. Muda si muda mnajua, kama wana kitu kidogo tu kichwani mwao, na kuanza kuzungumza na halmashauri na watu wa hapa karibu, na kusema, “Sasa mnajua nini? Jambo hili linapaswa kuwa tofauti.” Kama ninyi hamjazwa Roho, na mwe na mtu aliyejazwa

na Roho kabisa nyuma ya mimbara, muda si muda unajua, mtakuwa mnakubaliana na hoja zao. Labda si kizazi hiki; labda katika kizazi kijacho.

152 Na hivyo ndivyo ilivyoanza kuingia. Unaona? Kwa nini? Wao walikuwa wakisema, “Angalia hapa. Ni jambo zuri.” Ninyi, mngesikiliza.

153 Tuseme mtu aje hapa, ambaye angeweza kusema, “Kanisa hili ni dogo sana. Hebu na tujenge kanisa kubwa. Nitawajengeeni moja hapa, ni. . . litagharimu kiasi fulani cha fedha, dola nusu milioni. Litajengwa pale. Nitatangaza jambo hilo kwenye redio.” Wakifanya jambo hilo, basi wamewapata; mara tisa ya kumi, mnajua, mmoja wa watu wa aina hiyo. Muda si muda mnajua, basi, kama akifanya jambo hilo, yeye anaendeleza mambo kwa manufaa yake. “Hamwezi kusema kitu, kwa sababu Ndugu John Doe kule nyuma, yeye ndiye anayelidhamini kanisa hili.” Unaona? Na halafu mnampata maskini Ricky kutoka seminari fulani, anayejuu mengi juu ya Mungu kama Mhotentoti ajuavyo juu ya shujaa wa Kimisri, naye atakuja hapo na kubaliana na matakwa ya jamaa huyo, kwa sababu yeye humnunulia gari jipya wakati wote, anampa nafasi ya kuwa na gari la kuendesha huku na huko, na anamnunulia *hiki, kile, na kinginecho*.

154 Sasa, hivyo ndivyo hasa jambo hilo lilivyoanza. Kweli. Angalia, maarifa na akili! Wao wakasema, “Sasa angalieni hapa, si ni jambo zuri tu? Sasa, ninii. . . wanawake we—wetu, inaleta tofauti gani jinsi wanavyotengeneza nywele zao?” Lakini Biblia inasema tofauti ipo. Chukua tu jambo hilo moja, mbali na mamia ya mengine. Unaona? Tofauti ipo. Mungu alisema kuna tofauti, kwa hiyo ni tofauti.

155 Lakini, unaona, kama wakianza jambo hilo, na halmashauri ya wadhamini na mashemasi na kila kitu, muda si muda unajua, mchungaji aidha ataingia ama atatoka. Hivyo tu. Unaona, watu ndio waliopiga kura. Vema.

156 Sasa angalia, roho huyo alianza kutenda kazi, na kanisa ambalo liko namna hiyo, ambalo, lililo na watu wengi mashuhuri sana ndani yake, mambo mengi sana makubwa, na pesa nyingi sana zilizoanza, mpaka baada ya kitambo kidogo wakasikiliza jambo hilo na kushawishika na jambo hilo, kinyaa cha Ibilisi.

157 Na hilo ndilo jambo lenyewe hasa ambalo Hawa alitenda katika bustani ya Edeni. Sasa, mnasikia jambo hilo. Hiyo ni kweli. Angalia, mwanamke wa kawaida, Bibi-arusi wa Adamu, kabla yeye hajamjia kama mke, alishawishiwa na njama za Shetani dhidi ya Neno la Mungu, kwa kulihoji Hilo. Kabla Adamu hajaishi na Hawa kama mkewe, Shetani alimtangulia kwenye jambo hilo. Hiyo ni kweli. Mlisikia *Mti wa Bibi-arusi*, niliohubiri. Huo unanena habari zake, unaona. Vema. Sasa

angalia, hapo, Hawa alianguka kwa ajili ya kutoa hoja. Sasa yeye, Shetani, alijaribu kulijadili.

Akasema, “Lakini Bwana alisema . . .”

<sup>158</sup> Akasema, “Loo, unajua, lakini kweli Bwana hatafanya jambo hilo. Unaona? Wewe, unahitaji kuwa na maarifa. Unahitaji kujua jambo fulani. Mbona, wewe si kitu ila mtoto aliyebubu. Unaona? Unapaswa kujua jambo fulani.” Kama huyo si Shetani! Loo, jamani!

<sup>159</sup> Kama huyo si mmoja wa hawa, wa kisasa, unaona, “Loo, wao ni kundi la watakatifu wanaojivingirisha tu. Usiwajali, unaona. Usiende . . . Unaona?”

<sup>160</sup> Sasa, bibi-arusi wa kawaida, na wa kwanza wa jamii ya binadamu, kabla mumewe hajamjia, alianguka kutoka kwenye neema, kwa kusikiliza uongo wa Shetani, baada ya Mungu kumwekea ngome nyuma ya Neno Lake. Laiti angalika nyuma ya Neno, hangalianguka. Sasa hayo ni mambo ya kawaida, uone, mwanamke kawaida.

<sup>161</sup> Na laana ilikuwa ni nini, lile laana halisi la kutoka nyuma ya Neno la Mungu?

<sup>162</sup> Sasa kumbuka, yeye aliamini kama asilimia tisini na nane Yake. Lakini inataka tu kuachilia Jambo moja tu. Unaona? Yeye aliamini mengi sana ya jambo Hilo. Loo, bila shaka. Yeye alisema jambo Hili, na Shetani angekubali ya kwamba Hilo lilikuwa ni kweli. Kama anaweza tu kukupata kwenye kona moja, hivyo ndivyo tu anavyotaka. Unaona? Jambo tu unalopaswa kufanya ni kuitikisa risasi kidogo upande *huu*, na itakosa shabaha. Unaona? Ni hivyo tu. Sasa, yeye aliamini mengi sana Yake, lakini hata hivyo akalikosa.

<sup>163</sup> Sasa, na—na matokeo, kwa sababu yeye aliliacha Neno, kwa sababu ya hoja moja ndogo sana.

<sup>164</sup> Vema, tuseme sasa, “Vipi kuhusu wanawake?” Au, “Kwa nini unataka kuzungumza juu ya jambo kama hilo?” Hakika lo lote la hayo mambo madogo. “Kuna tofauti gani, kama ikiwa ni ushuhuda wa kwanza?” Kuna kitu kwake! Una- . . .

<sup>165</sup> Halina budi kunyoshwa. Tumelidhania Hilo, katika nyakati saba nzima za kanisa, karibu. Lakini saa imewadia wakati Mungu analinena. Wala Yeye halineni tu, lakini analionyesha, na kulithibitisha, na kulihakikisha. Hiyo ni kweli. Kama Yeye hafanyi hivyo, basi si la Mungu, hivyo tu. Mungu husimama nyuma ya Neno Lake.

<sup>166</sup> Angalia sasa. Sasa, mwanamke wa kawaida alisababisha mauti ya kawaida, kwa sababu alisikiliza hoja, kujifanya mwerevu, kujifanya mwerevu badala ya kukaa nyuma ya Neno na kufanya yale aliyoambiwa na Mungu. Alitaka hekima, na kuwa na hekima. Naye akasikiliza hoja, na—na akaipoteza jamii yote ya mwanadamu. Unaona?

167 Sasa, wakati huu, yule mwanamke wa kiroho, Bibi-arusi wa Kristo aliyeanza kwenye Siku ya Pentekoste, na Kanisa la mwanzoni la mitume, alipoteza jambo lile lile kwenye Baraza la Nikea. Lee, unajua jambo hilo ni kweli. Na kwenye—kwenye Baraza la Nikea, wakati alipobadilishana na haki zake za kiroho za mzaliwa wa kwanza, apate kuchukua makanisa makubwa ya Konstantino na vitu alivyowapa kule, na aliua haki zake za Kimaandiko za mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya lundo la mafundisho ya sharti ya Kiroma. Sasa, hilo ni zito kwa Mkatoliki. Lakini Waprotestanti wamefanya jambo lile lile, na wanawakilishwa, katika Biblia hapa, kama binti “wa malaya, wa kahaba.” Hiyo ni kweli kabisa, kila mmoja wao! Hakuna udhuru.

168 Lakini kutoka katika hao daima kumekuwako na wachache waliosalia, wakati wote, ambao wanafanyiza Bibi-arusi.

169 Angalia, yeye alipoteza haki zake za mzaliwa wa kwanza, unaona, kabla mume wake hajamfikia. Unaona? Kabla ya arusi, alipoteza usafi wake.

170 Na sasa mnakumbuka kule, yeye alisema, “Nimeketi kama malkia. Sina haja ya kitu,” katika ule Wakati wa Laodikia pale. “Mimi ni tajiri na nimejitajirisha, na kadhalika. Na, loo, ulimwengu mzima unaniheshimu. Mimi ndiye lile kanisa lililo kuu, takatifu, na kadhalika. Sisi tuko *hivi*,” wakati ule wote mzima.

171 Naye akasema, “Hujui ya kuwa wewe u uchi, kipofu, mwenye mashaka, mnyonge, maskini, wala hujui.” Hivyo ndivyo hali ilivyo. Sasa, kama Roho Mtakatifu alisema hali ingekuwa namna hiyo katika siku za mwisho, iko hivyo! Hakuna njia ya kuepuka jambo hilo. Hivyo ndivyo ilivyo.

172 Sasa angalia. Sasa, wakati alipouza haki zake za mzaliwa wa kwanza huko nyuma, haki yake ya usafi, ya Neno, alifanya nini? Wakati Hawa alipofanya jambo hilo, alipoteza viumbe; viumbe vyote vilianguka chini yake.

173 Sasa angalia, na wakati kanisa lilipofanya jambo hilo, lilipokubali mafundisho ya sharti badala ya Roho na Neno, lililaani utaratibu wote. Utaratibu wote wa kimadhehebu uliopata kuwapo, ama utakaopata kuwapo, ulilaaniwa pamoja nao, na kuanguka, kwa maana hakuna njia nyingine.

174 Unapolikutanisha kundi la watu, kufikiria jambo lo lote, mmoja ameweka kichwa *hivi*, na mmoja ameweka kichwa *vile*, na mwingine ameweka kichwa *hivi*. Nao wanaweka mambo hayo pamoja na kuyatikisa, na, yanapotokea, hicho ndicho unachopata.

175 Hivyo ndivyo walivyofanya hasa huko kwenye Baraza la Nikea. Hivyo ndivyo hasa wanavyofanya kwenye la Methodisti, la Presbiteri, kanisa la Kristo, na hayo mengine. Na hakuna mtu, haidhuru Mungu anamfunulia nini, huna budi kulifundisha



jinsi kitambulisho chao, kanuni—kanuni yao isemavyo, la sivyo watakufukuza. Sasa, usiniambie. Nimekuwa kule, unaona, nami najua jambo hilo.

<sup>176</sup> Na hivyo ndivyo ilivyotukia hasa, kwa hiyo jambo lote limelaaniwa. Si ajabu malaika alisema, “Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msipokee mapigo yake.” Kwa sababu, yeye ataninii. . . Amelaaniwa, na hana budi kupata laana ya ghadhabu ya Mungu juu yake, kwa sababu aliuza usafi wake na haki zake. Unaona? Lakini. . . Loo, jamani!

<sup>177</sup> Lakini, kumbukeni. Tukiona hali hiyo yote, lakini hata hivyo Mungu aliahidi, katika Yoeli 2:25, kama ukitaka kuliandika, “Katika siku za mwisho. . .”

<sup>178</sup> Wakati aliposema, “Yaliyosazwa na tunutu, yaliliwa na madumadu; yaliyosazwa na madumadu, yameliwa na nzi—nzige; yaliyoliwa na nzige. . .” Kuendelea mbele tu, mdudu baada ya mdudu, alikuwa amekuwa na kulila Kanisa hilo mpaka hatimaye halikusalia kitu ila kisiki. Angalia! Yaliyosazwa na Waroma, yameliwa na Waluteri; yaliyosazwa na Waluteri, yameliwa na Wamethodisti; na yaliyosazwa na Wamethodisti, yameliwa na Wapentekoste; unaona, mpaka limefikia kwenye kisiki.

<sup>179</sup> Na unajua nini? Hebu wachukue hao wadudu hapo ndani, nzige na madumadu, na kadhalika, na uwafuatilie katika ki—kitab, na uone. Ni mdudu yule yule tu katika hatua mbalimbali tu.

<sup>180</sup> Shikilia jambo lako. Vivyo hivyo na Mihuri hii! Ni wadudu wale wale. Mtaona jambo hilo tutakapolielezea, kwa hiyo nitawaambia sasa. Ni mdudu yule yule, wakati wote. Hao wadudu wanne; wanne hapa. Na ndio hao hapo, ni kitu kile kile. Ni roho yule yule. Yaliyosazwa na mmoja, huyo mwingine alikula; na yaliyosazwa na *huyu*, huyo mwingine alikula; namna hiyo, mpaka wakaufikisha kwenye kisiki.

<sup>181</sup> Lakini Yoeli alisema, “Nitawarudishia, asema Bwana, miaka yote iliyoliwa na madumadu.”

<sup>182</sup> Ni kitu gani? Yeye atafanyaje jambo hilo; kama lilianza, upinga-Kristo, kwa kupinga mafundisho ya Kristo, ambapo walikubali mafundisho ya sharti badala ya Neno? Na kwa miaka kadha wa kadha watengenezaji waliingilia, kama ilivyosema Biblia.

<sup>183</sup> “Lakini katika siku ya mwisho, katika kupigwa. . .” Ufunuo 10:1-7, Yeye alisema, “Siri za Mungu zingetimizwa katika siku za mwisho, katika kupigwa kwa baragumu ya malaika wa saba.” Malaki 4, ilisema ya kwamba Yeye “Angemtuma Elisha kabla haijaja ile siku ya uovu juu ya nchi, wakati atakapoiteketeza kama tanuru. Naye angerudisha, na kuwarudisha wa—watoto kwenye Imani ya baba zao,” ile Imani asili, ya mitume, ya kipentekoste iliahidiwa kurudishwa. Sasa, hilo ni dhahiri kama vile Maandiko yanavyoweza kulisema. Sasa limeahidiwa. Na

kama tuko katika siku za mwisho, jambo fulani halina budi kutukia. Unaona? Na linatukia, nasi tunalionna.

<sup>184</sup> Angalia utatu wa Shetani. Mtu yule yule akija; amefanyika mwili tu, toka mmoja kwenda kwa mwingine. Hivyo ndivyo wadudu hao walivyofanya, hao wadudu, mmoja kwa mwingine, hasa. Unikolai, “upinga-Kristo wa kiroho.” Papa, “nabii wa uongo.” “Mnyama,” Ibilisi mwenyewe, aliyefanyika mwili. Hawezi kufanya jambo hilo. . .

<sup>185</sup> Sasa, weka jambo hilo niani mwako sasa, unapofuatilia jambo hili. Utaona wapanda farasi hawa wakija moja kwa moja kwenye jambo hilo. Unaona, ninakuwekea picha hapa. Kama nilikuwa nimeichora kwenye ubao, ungaliweza kufahamu vizuri zaidi. Unaona, ninaangalia.

<sup>186</sup> Kwanza, sasa. Kumbuka jambo hili. Jambo la kwanza alilo, yeye ni “roho wa mpinga-Kristo.” Yohana alisema hivyo. “Enyi watoto wadogo, roho ya mpinga-Kristo tayari inatenda kazi katika wana wa kuasi.” Unaona, jambo hilo lilikuwa limeanza kuanza. Na baadaye likawa kwa namna fulani “msemu,” katika wakati wa kanisa uliofuata. Na katika wakati wa kanisa uliofuata, likawa “fundisho.” Na wakati wa kanisa uliofuata, yeye “alivikwa taji.” Sasa hilo si ni jambo dhahiri tu kama kusoma mahali po pote ungaliweza kulisoma? Unaona? Unaona, huyo hapo anakuja.

<sup>187</sup> Sasa, kwanza, yeye aliitwa (nini?) “roho ya mpinga-Kristo,” kwa sababu alikuwa akipinga Neno. Hicho ndicho kilichoanzisha jambo hilo. Hicho ndicho kilichofanya jambo hilo lote, ilikuwa ni kuliacha Neno la Mungu. Si kwa sababu huenda Hawa alimpiga Kaini kofi siku moja. Unaona? Hicho sicho kilichosababisha jambo hilo. Jambo la kwanza lililosababisha jambo hilo lote, ilikuwa ni kwamba yeye aliliacha Neno. Yeye aliliacha Neno. Na jambo la kwanza, lililoanzisha umalaya katika kanisa la Mungu aliye hai, Bibi-arusi wa Kristo, aliliacha Neno na kukubali fundisho la sharti la Roma badala ya Neno la Mungu. Ni kitu gani kimepata kila madhehebu? Lilifanya jambo lile lile.

<sup>188</sup> Sasa, lakini aliahidi ya kwamba katika siku za mwisho Yeye angefanya njia ya kurudisha tena. Neno la Bwana lingeshuka duniani, kama Yeye alivyofanya pale mwanzo, na, loo, na litarudisha (nini?) kile kilichosababisha jambo hilo. “Dhidi ya Neno.” Na jamaa huyu anapaswa kufanya nini atakapokuja, akiwa ametiwa mafuta ya Roho wa Mungu? Yeye “anairudisha tu Imani ya watoto irudi kwenye ile ya baba zao.” Hivyo ndivyo anavyoirudisha. Nawe unapata Neno lili hili, katika mahali pale pale lilivyo *Hapa*, litafanya jambo lile lile.

<sup>189</sup> Yesu alisema, “Kama mtu ye yote akiwa ni Wangu! Naye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya pia.” Na wakati walipomwambia afanye mambo fulani, Yeye

alisema, “Ninatenda tu yale Baba anayonionyesha. Sitendi neno mpaka nilione, kwanza. Lile nionalo Baba akitenda, ndilo nitendalo vile vile. Baba anatenda kazi, na basi ninatenda kazi hata sasa.” Unaona? Huoni jambo hilo? Mbona, ni kama tu kusoma gazeti. Unaona?

Sasa, sasa, kwanza, basi, yeye akawa “mpinga-Kristo.”

<sup>190</sup> Sasa, yeye hangeweza kuwa mpinga-Kristo katika roho tu. Halafu, yeye alifanyika mpinga-Kristo, na roho huyo akamchukua mtu aliyefundisha mambo yale yale ambayo roho yule wa mpinga-Kristo alikuwa akifanya, na ndipo akawa “nabii wa uongo,” kwa roho wa mpinga-Kristo. Sasa vipi kuhusu mtu katika madhehebu? Ni juu yako. Sijui unavyofikiri juu ya jambo hilo. Vema.

<sup>191</sup> Sasa, hatimaye, yeye anakuwa “mnyama.” Sasa ngoja, nasi tutapata jambo hilo baada ya kitambo kidogo, unaona. Vema.

<sup>192</sup> Sasa, kwa maana ndivyo ulivyo utatu wa Shetani; Shetani, daima. Shetani, “roho ya mpinga-Kristo.” Roho ya mpinga-Kristo, aliyefanyika mwili, “nabii wa uongo.” Halafu, anakuwa “mnyama.” Unaona? Wakati . . . Si pepo, yule aliyekuwa katika yule mpinga-Kristo; lakini wakati Shetani mwenyewe atakapofukuzwa, anashuka chini na kuchukua mahali alipokuwa anakaa huyo pepo. Ibilisi, wakati huo, ndipo Ibilisi anafanyika mwili katika mwanadamu. Inajirudia tu yenyewe.

<sup>193</sup> Hivyo ndivyo alivyokuwa Yuda Iskariote. Naye alifanya nini? Je! yeye alikuwa mmoja wa hao watu waliompinga Kristo? Mbona, alikuwa mweka hazina, akatembea pamoja Naye. Bila shaka. Alitembea moja kwa moja pamoja nao. Akatoka akaenda huko na kutoa pepo, na kufanya vile yale waliyofanya wao.

<sup>194</sup> Na Kristo alikuwa Mungu aliyefanyika mwili; Mungu, aliyefanyika mwili, Imanueli. Naye Yuda alikuwa mwana wa upotevu. Naye Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Mungu aliyefanyika mwili; Ibilisi aliyefanyika mwili.

<sup>195</sup> Watu wengine wanaona misalaba mitatu tu wakati huo. Kulikuwa na minne. Kulikuwako na mitatu huko Gologotha, tunayoiona. Hiyo ilikuwa ni Yesu katikati, mwizi kwenye mkono Wake wa kushoto, na mwizi kwenye mkono Wake wa kulia.

<sup>196</sup> Basi angalia. Mwizi mmoja alimwambia huyo mwingine, ama alimwambia Yesu, “Kama . . .” Sasa, unajua Yeye ni Neno. Lakini, “Kama Wewe ni Neno, mbona usijiokoe mwenyewe? Mbona usifanye kitu juu ya jambo hilo?”

<sup>197</sup> Hilo ndilo jambo lile lile leo. Hivi hamjasikia hawa ibilisi wa kale wakija, kusema, “Kama unaamini katika kuponya Kiungu, *haya* hapa macho ya mtu fulani, mbona usiyafungue?” “Nipige kwa upofu! Nipige kwa upofu!” Ibilisi yule yule wa kale. Unaona? “Shuka msalabani, tutakuamini.” “Kama Wewe

ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate.” Ibilisi yule yule.

198 Wewe jiondokee uende zako tu, unaona. La. Hivyo ndivyo Yesu aliyofanya. Yeye hakufurahisha mtu ye yote wao kwa vitimbi.

199 Waliweka kitambaa juu ya mkono Wake . . . kwenye macho Yake ya thamani, namna *hiyo*. Na wakachukua fimbo, na kumpiga utosini. Kasema, “Tuambie! Kama wewe ni nabii, sasa tuambie ni nani aliyekupiga.” Wakabadilishana fimbo, mmoja kwa mwingine. “Sasa tuambie ni nani aliyekupiga, nasi tutaamini Wewe ni nabii.” Hakufungua kinywa Chake hata kidogo. Aliketi tu pale. Unaona? Yeye haburudishi watu kwa michezo. Anafanya tu yale asemayo Baba, unaona. Unaona? Anawaacha waendele. Wakati wao unakuja. Usijali. Naam, bwana. Sasa, waligusa vazi Lake, hawakusikia nguvu yo yote.

200 Lakini maskini kijana mmoja mwanamke, alikuwa na haja, aligusa tu vazi Lake. Akageuka na akasema, “Ni nani aliyenigusa?” A-ha. Ni nini? Mguso tofauti. Inategemea jinsi unavyomgusa Yeye, unaona, unaona, kile unachoamini. Sasa, unaona?

201 Sasa, kwa kuwa Shetani ataninii . . . amechukua mwili, kutoka mpinga-Kristo akawa nabii wa uongo sasa. Na katika siku za Wayahudi, ni “mpinga-Kristo,” kati ya kanisa la mwanzoni. Katika zile nyakati za giza, yeye akawa “nabii wa uongo,” kwa ulimwengu. Unamwona pale na “kikombe chake cha maovu”? Sasa, hiyo ni kwa wakati wa kanisa sasa.

202 Lakini katika ule wakati baada ya Kanisa kwenda Nyumbani, yeye anafanyika mnyama, anakuwa Ibilisi aliyefanyika mwili, lile joka jekundu lenyewe. Loo, jamani! Huwezi kuona ninalomaanisha? Yeye anafanyika mwili katika watu wake wakati huo. Amewafunga watu wake kwa nguvu zake. Nabii wa uongo amewatabiria mpaka wakaingia kwenye jambo hilo. “Kuwaletae nguvu ya upotevu, kuamini uongo ili wahukumiwe nao.” “Wakikana Neno; wakiwa na mfano wa utauwa.”

203 Mungu hutenda kazi, mahali Pake, katika utatu. Kuhesabiwa haki; kutakaswa; na kufanyika mwili Mwenyewe katika watu Wake, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

204 Jambo lile lile, Ibilisi yuko tu katika mfano, wa Kristo. Loo, Shetani hufanyika mwili . . . Sasa angalia. Shetani . . .

205 Wakati Yesu anapofanyika mwili katika watu Wake, Uhai ule ule uliokuwamo katika Kristo uko ndani ya mtu huyo.

206 Ingekuwaje kama ungetoa uhai kutoka katika mzabibu na uweke kwenye mboga? Haungezaa maboga tena; ungezaa zabibu. Vipi kama ungetoa uhai kutoka katika mwembe na

kuuweka katika mpea? Ungezaa mapea? La. Ungezaa maembe. Uhai ndio unaonyesha ni kitu gani. Unaona?

<sup>207</sup> Unaposema, unapowasikia watu wakisema wana Roho Mtakatifu, nao wanalikana Neno hili, kuna kasoro. Roho Mtakatifu ndiye aliyeliandika Neno hilo.

<sup>208</sup> Na Yesu alisema jambo hili, “Kama mtu ana Roho Wangu ndani yake, atafanya kazi Zangu.” Unataka kusoma jambo hilo? Unataka kuliandika? Ni Yohana Mtakatifu 14:12. Naam. Vema. “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye naye atazifanya. Hata nyingi kuliko hizi atafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba.” Unaona? Ndipo anamtakasa na kumsafisha, ili aweze kusimama mbele za Mungu. Hilo tone la wino linaanguka pale, na kumvusha upande wa pili wa lile shimo. Unaona?

<sup>209</sup> Sasa angalia. Shetani, wakati anapofanyika mwili katika raia wake, wanafanya kazi aliyofanya. Hamwoni? Alifanya nini? Alikuwa moja kwa moja kwa mwanamke yule asiye na hatia, kumdanganya. Na hivyo ndivyo hasa baadhi ya hawa pepo wanavyofanya, wanafika moja kwa moja mahali fulani na kusema . . . Maskini mchungaji anaanza, huko nje mahali fulani; anakuja na kusema, “Loo, laiti ungaliungana tu na sisi!” A-ha! A-ha! Kazi ile ile ya ibilisi. Sasa, hiyo ni Kweli! Na Shetani anapofanyika mwili katika kanisa lake, kuwa ibilisi, basi hao ndio wanaoua kinyama na kuua, na kadhalika. Kwa sababu, Shetani ni muuaji, kwanza; mwongo na . . . Unaona? Vema.

<sup>210</sup> Shetani anafanya nini wakati anaponinii, anapofanyika mwili kati ya watu? Ni kazi yake kuwa mwerevu. Yeye ni mwerevu. Ichunguze Biblia, na unionyeshe mahali ambapo Mungu alipata kuhangaika na watu wenye akili. Patafute, uone kama daima si watu wenye akili ambao wamepagawa na pepo. Ni neno kubwa, lakini ni kweli. Ninawasai kuchukua u—ukoo, kutoka Habili mpaka Kaini; na, hivyo vizazi kumi na vinne, uvifuatilie, uone ni upande gani uliokuwa na akili, na ni upi uliokuwa mnyenyekevu. A-ha.

<sup>211</sup> Kwa nini Yesu hakuwachagua watu kama hao? Alichukua wavuvi na wanaume ambao hawakuweza hata kuandika jina lao wenyewe, kuwafanya kiongozi wa Kanisa Lake. Hiyo ni kweli. Maarifa si—si kitu; yana—yanapingana na Kristo. Hekima ya kilimwengu inapingana na Kristo, daima. Yesu hakutuambia kamwe twende tukajenge maseminari; Yeye kamwe hakutuambia hivyo; kuwa na shule za Biblia. Alisema, “Hubirini Neno! Hubirini Injili!” Na halafu kama alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” unaona, itakubidi kuwa na . . . Kwa maneno mengine, Yeye alisema, “Enendeni mkaonyeshe Nguvu za Mungu, kwa mataifa yote.”

212 Sasa angalia. Kazi ya Shetani ni kupotosha Neno la Mungu, kwa hoja za maarifa. Loo, jamani! Loo! Ndipo anawatia alama raia wake, kwa kulikataa Neno la asili. Sasa hebu hilo . . .

213 Je! mtani—mtani—mtanivumilia kidogo tu zaidi, na mpate jambo hili? Hili, siwataki mkose jambo hili. Hebu niwaonyesheni mfano, ili mweze kuliona lote katika mfano na katika Neno, na kila kitu. Ha—hamwezi . . . Hampaswi kuondoka mwende mmechanganyikiwa.

214 Katika Agano la Kale, wakati mtu alipouzwa katika utumwa. Ulikuwa mwaka wa yubile, kila baada ya miaka hamsini. Mwaka wa arobaini na tisa, na halafu mwaka wa yubile. Na wakati mtumwa aliposikia jambo hili, na alitaka kuwa huru, kuna—hakuna kitu kinachoweza kumzuia kuwa huru. Anaweza kutupa jembe lake chini, na kusema, “imetosha,” arudi nyumbani. Baragumu ilipigwa. Hiyo ni kweli.

215 Lakini kama hataki kwenda, naye ametosheka na bwana wake wa watumwa, basi anapelekwa he—he—hekaluni, nao wanachukua msharasi . . . Mnajua msharasi ni kitu gani. Nao wanatoboa sikio lake, na kufanya tundu kwenye sikio lake. Na ni alama, ya kwamba hawezi kamwe kurudi. Hiyo ni kweli? Hana budi kumtumikia bwana huyu wakati wote. Sijali ni mara ngapi zaidi yubile italia, cho chote kitakachotendeka. Yeye kabisa ame—ameza haki zake za mzaliwa wa kwanza, za kuwa huru.

216 Na wakati mtu anapokataa Kweli ya Injili, Shetani anamtia alama (wapi?) sikioni. Yeye humziba masikio ili asiweze kusikia Kweli tena, naye amekwisha. Anakaa na kundi alilo nalo, kama hatasikia Kweli. La.

217 “Utajua Kweli, na Kweli itawaweka huru.” Unaona, Kweli huweka huru.

218 Mungu huwatia Wake alama wanapokuja. Mungu hutia Wake alama kwa kuthibitisha Neno Lake la ahadi kupitia kwao. Hiyo ni kweli kabisa, Yohana Mtakatifu 14:12. Na jambo lingine, unataka kuliandika, Marko 16. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

219 Sasa hebu na tuchukue jambo hilo tu, kwa dakika moja. Je! Yeye alikuwa akitania? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Je! alimaanisha tu ninii . . . Alimaanisha ni mitume tu, kama vile wengine wangetuambia? [“La.”]

220 Angalia. Soma msingi wake. “Enendeni . . .” Wapi? [Kusanyiko linasema, “Ulimwenguni mwote.”—Mh.] “Ulimwenguni mwote.” “Kuhubiri Injili hii kwa . . .” Akina nani? [“Kila kiumbe.”] “Kila kiumbe.” Hata haijafikia theluthi moja ya njia bado. “Ishara hizi zitafuata katika ulimwengu wote, kwa kila kiumbe, po pote Injili hii itakapohubiriwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” si kwa kundi moja dogo tu.

221 Kama jamaa fulani wakati mmoja alivyokuwa ananiambia, “Mungu aliwapa wale mitume kumi na wawili peke yao karama za uponyaji. Na . . .” Loo! Kwa hiyo, wengi wa ndugu walikuwa wameketi hapa wakati alipoinuka kusema jambo hilo, unaona. Alipata ya kutosha, katika dakika chache.

222 Kwa hiyo sasa angalia, “Ulimwenguni mwote, kwa kila kiumbe, ishara hizi zitafuatana.”

223 Usichukue alama ya Shetani ya kutokuamini. Sasa, yeye ataiweka juu yako usiku wa leo, kama anaweza kufanya jambo hilo. Atakusukumia ukutani, nawe ungetoka na kusema, “Sijui juu ya jambo hilo.”

224 Wewe nenda nyumbani ukasome jambo Hilo, na halafu uwe mnyofu, na uombe. Maana, kila kitu ni cha Kimaandiko ka—kabisa katika wakati huu wa sasa hivi, kipindi hiki cha majira haya yaliyowekwa wakfu. Imekuwa hivyo kwa miaka mingi, imethibitishwa, tumefikia jambo hilo. Na wakati ndio huu. Wakati ndio huu.

225 Na sasa usimwache ashindilie kitu hicho sikioni mwako, alama yake ya kutokuamini. Unaona? Maana, yeye alikuwa asiyeamini, kwanza. Alitilia jambo hilo shaka. Vema. Loo, hata usininii . . . Usimwache ayachukue Maandiko, kwa maarifa yake, na—na kuyageuza na kuyapotosha kwa maarifa yake mwenyewe, kuingia katika nguvu za hoja. Wewe uwe tu mnyenyekevu, na useme, “Mungu alisema hivyo, na ni hayo tu.” Sasa, loo, hebu . . .

226 Tutachelewa sana, kwa hiyo afadhali tusimame papa hapa na—na kuanza.

227 Sasa hebu twende kwenye Muhuri wa pili. Wakati Mwana-Kondoo aliyechinjwa, aliyefufuka alipoufungua huu, na yule Mwenye Uhai wa pili, aliyefanana na ndama, akasema, “Njoo, uone siri ya Muhuri huu ni nini.” Unaona? Sasa tunalipata. Mwana-Kondoo, kumbuka, inabidi afungue kila Muhuri. Na yule Mwenye Uhai wa pili . . .

228 Kama ulichunguza jambo hilo, katika utaratibu ambao ndio kwanza tupitie, pamoja na nyakati za kanisa, jambo lile lile. Wa pili . . . Wa kwanza alikuwa ni simba; wa pili alikuwa—alikuwa ni . . . alikuwa kama ndama, ama maksai, ama kitu fulani unaona.

229 Na Mwenye Uhai huyu alisema, “Njoo, uone,” sasa, na wakati Mwana-Kondoo alipoufungua ule Muhuri. Na, halafu, akaenda kuona. Na wakati alipoingia, ni jambo gani lililotukia? Hebu na tuone aliona kitu gani sasa. “Njoo, uone.” Kuna siri iliyotiwa muhuri hapa, ambayo imekuwa hapa sasa kwa miaka elfu mbili, hivi. Hebu tuone ni kitu gani.

230 Sasa tunaona hapa ya kwamba yeye aliona (kitu gani?) farasi mwekundu akienda mbele. Sasa, ninavyofahamu jambo hili, nijuavyo mimi, huu upanga mkubwa aliokuwa nao mkononi

mwake . . . Sasa tuna kama vitu vitatu vya kuangalia sasa, kwa kama dakika kumi na tano zifuatazo, dakika ishirini. Hebu tu tusome na tuone jambo analosema hapa. “Na akatoka . . .” Kifungu cha 4.

*. . . Akatoka farasi mwingine, mwekundu sana, (wa kwanza alikuwa ni mweupe): na yeye aliyempanda alipewa mamlaka kuiondoa amani katika nchi, . . . watu wauane, naye akapewa upanga mkubwa.*

<sup>231</sup> Sasa kuna mifano hapa, nasi tunataka kuiangalia kwa makini sana. Lakini, ninavyofahamu, ni juavyo mimi kabisa sasa, unaona, Yesu alibashiri jambo lile lile katika Mathayo 24. Unaona? Alisema, “Sasa mtasikia habari za vita na matetesi ya vita, na vita tu na matetesi ya vita, na vita. Na, lakini,” kasema, “mambo haya yote bado siyo. Unaona, ule wakati bado.” Unaona, walimwuliza Yesu maswali matatu. Unaona? Naye akawajibu kwa maswali matatu.

<sup>232</sup> Hapo ndipo ndugu wengi walipochanganyikiwa, wakijaribu kuweka . . . Ndugu wa Sabato, juu ya hizo, siku ya saba na kadhalika, kule nyuma, ninii . . . “Ole wake anayezaa, aamwishaye, na malango yatafungwa katika siku ya sabato,” na mambo kama hayo. Jamani! Hilo hata halihusiani na swali hilo kamwe, unaona, hata kidogo. Unaona?

<sup>233</sup> Yeye alikuwa akijibu yale waliyouliza, lakini haku—hakuyaweka yote kwenye siku za mwisho. Alisema, “Mtasikia . . .” Sasa tunajishughulisha na jambo hili moja hapa. Tutafikia mengine yake zaidi, katika masiku machache yajayo. Yeye alisema, “Mtasikia habari za vita, na matetesi ya vita, na kadhalika. Ndipo haya yote si . . . Unaona, ndipo wao wataninii—wao watarudi tena, ndipo watawasaliti, na kadhalika namna hii. Na yote, yote hayo hayajatimia bado.”

<sup>234</sup> Lakini alipofikia katika wakati alipokuwa azungumze nao juu ya yale waliyomwuliza habari zake, “mwisho wa dunia.”

<sup>235</sup> “Mambo haya yote yatakuwa ni lini, ambapo halitasalia jiwe juu? Ni nini dalili yake? Ni kule kuja kutakuwa ni lini, mwisho wa dunia?” Unaona, wao walimwuliza mambo matatu?”

Ndipo wakati alipofikia kwenye, “Mwisho wa dunia?”

<sup>236</sup> Alisema, “Mtakapona mtini ukichanua majani yake, sasa mnajua ya kwamba wakati umekaribia. Na amin nawaambieni, ya kwamba, kizazi hiki hakitapita mpaka yote yatakapotimia.” Jinsi kafiri, asiye na ufafanuzi, anavyopenda kushikilia jambo hilo! Unaona? Yeye alisema, “Kizazi hiki,” si kizazi kile alichokuwa akinena nacho, “kizazi kile kilichoona mtini ukichanua majani yake.”

<sup>237</sup> Sasa nataka kukuliza tu jambo fulani. A—angalia tu jambo fulani papa hapa usoni. Israeli sasa, kwa mara yake ya kwanza katika miaka elfu mbili na mia tano, ni taifa. Bendera ya kale



sana kuliko zote ulimwenguni inapepea juu ya Yerusalemu usiku wa leo. Israeli wako katika nchi ya uenyeji wao.

238 Kulikuwa na ndugu hapa wakati mmoja aliyetaka kuwa mmishenari, alijisikia aende kama mmishenari kwa Wayahudi. Nikasema, “Unaweza kumpata mmoja pengine.” Loo, watu wanafikiri, taifa zima! La, bwana.

239 Israeli itaongolewa kama taifa, si kama mtu binafsi. “Taifa litazaliwa katika siku moja.” Hilo ni Israeli. “Israeli wote wameokolewa.” Kumbukeni tu jambo hilo. Paulo alisema hivyo, “Israeli wote wameokolewa.” Sasa angalia, “Israeli wote.” Hiyo ni kweli kabisa.

240 Sasa angalia jambo hili. “Lakini,” Yeye alisema, “mtakapooni mtini, na miti mingine yote, ikichipua majani yao.” Sasa angalia. Hapajakuwapo na wakati, kwa miaka elfu mbili na mia tano, ambapo Israeli wamewahi kuja kwenye nchi ya uenyeji wao. Tuna ile sinema fupi, ya *Usiku wa Manane Kasoro Dakika Tatu*, unajua. Huyu hapo, taifa, nyota yenye ncha sita ya Daudi, ikipepea, na mambo haya yote.

241 Kumepata kuwapo na wakati ambapo madhehebu yamekuwa na miamsho kama ambayo wamekuwa nayo katika miaka michache iliyopita? Sasa soma tu jambo hilo. Tumewasili nyumbani.

242 Ni wakati gani madhehebu yalipata kusitawi chini ya huduma ya mtu ye yote, kama vile yalivyofanya chini ya huduma ya Billy Graham; Wamethodisti, Wabaptisti, na kadhalika? Ni lini kuliwahi kutokea mtu, ichunguzeni historia yenu, aliyepata kwenda kwenye kanisa baridi, mwenye jina linaloishia na h-a-m, hapo nyuma? Nawaulizeni tu. I-b-e . . .

243 I-b-r-a-h-i-m-u. Sasa angalia, jina la Ibrahimu lina herufi saba, A-b-r-a-h-a-m.

244 Lakini Ndugu yetu Billy Graham, ana G-r-a-h-a-m, sita, si saba. Duniani, huko ndiko anakohudumu, kwenye kanisa baridi.

245 Kanisa baridi, lilikuwa ni Lutu, katika Sodoma. Na wakati jamaa huyu aliposhuka akaenda kule na kuhubiri, na akawapofusha kwa Injili.

246 Lakini kulikuwako na Mmoja Ambaye alikaa na Ibrahimu, naye Ibrahimu alimwita, “Elohimu, Bwana.” Sasa wakati Ibrahimu alipowaona watatu wakija, alisema, “Bwana wangu.”

247 Lutu alipowaona wawili wakija, alisema, “Bwana zangu.” Hiyo hapo tofauti yenu. Unaona kazi yenu ya utatu? Unaona?

248 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu.” Unaona jambo hilo? Angalieni. Hesabuni.

249 Sasa, kuna Mmoja aliyekuwa kwenye Kanisa la kiroho, Bibi-arusi, Ibrahimu, huyo hakuwa huko—huko Sodoma, kwanza.

Na angalia jambo alilotenda. Yeye hakuhubiri kwa namna wao walivyohubiri. Aliwafundisha, lakini basi walitenda ishara hizo mbele yao. Alifanya ishara ya Masihi. Alikuwa ameelekeza mgongo Wake hemani, Naye akasema, "Ibrahimu." Sasa kumbuka, jina lake halisi, siku chache kabla ya hapo, lilikuwa ni Abram. Lakini Yeye anasema, "Ibrahimu, yuko wapi mke wako, S-a-r-a?" Siku chache kabla ya wakati huo, aliitwa S-a-r-a-i.

Ibrahimu akasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

<sup>250</sup> Naye akasema, "Ibrahimu, Mimi. . ." Hicho hapo kijina chako cha kumtaja mtu tena. "Nitakurudia kulingana na ahadi niliyokupa." Unaona ilikuwa ni kitu gani. Unaona? Mwanamume, akiwa na mavumbi kwenye nguo Zake, akila nyama ya ndama, na akinywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na akila ugali wa mahindi. Naam, bwana. Mungu, Elohimu, akidhihirishwa katika mwili!

<sup>251</sup> Aliahidi, katika siku ya mwisho, kujidhihirisha Mwenyewe katika mwili tena! Angalia.

"Ibrahimu, yu wapi mkeo, Sara?"

"Yumo hemani, nyuma Yako."

Kasema, "Nitakurudia."

<sup>252</sup> Na bibi huyo, bila shaka, akiwa na umri wa miaka mia moja, kwa namna fulani alicheka kifichifichi; huko nyuma hemani sasa, nyuma ya mapazia huko hemani. Akasema, "Mimi, mwanamke mkongwe." Vema, ilikuwa imekwisha koma kwao, kama mume na mke, kwa miaka mingi, unajua, maana alikuwa na umri wa miaka mia moja, na—na—na mke alikuwa na tisini. Kasema, "Jambo hilo halitatukia kamwe."

<sup>253</sup> Naye akasema, "Kwa nini amecheka?" Whiu! akiwa amegeuza mgongo Wake kuelekea hemani, "Kwa nini amecheka, akisema, 'Mambo haya yanawezekanaje?'" Unaona, Yeye alimwonyesha ishara.

<sup>254</sup> Sasa Yeye anaahidi ya kwamba jambo hili litajirudia katika siku za mwisho, tena.

<sup>255</sup> Na hao watu wawili wakashuka wakaenda kule na kuhubiri Neno, na kuwaambia watoke hapo; mahali hapo patateketezwa, na kadhalika. Na paliteketezwa. Naye Lutu akasitasita kutoka; kanisa baridi, kule chini katika dhambi, na katika matope, lakini hata hivyo likisonga mbele kwa shida katika mipango yao ya kimadhehebu. Lakini Bibi-arusi. . .

<sup>256</sup> Huyu mtu huyo mmoja kamwe hakuwaendea. Alienda tu na kuwaita wale walio mfano wa Bibi-arusi. Sasa tuko katika siku za mwisho. Unaona? Sasa angalia.

"Wewe ulisema pale, 'Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili?'"

257 Yesu alisema, Yeye Mwenyewe, “Mnanihukumuje?” Kasema, “Je! haikuandikwa katika Biblia yenu, sheria zenu, ya kwamba wao, hao manabii, ambao walijiliwa na Neno la Mungu. . .” Yesu alisema, “Neno liliwajilia manabii,” maana Yeye alikuwa wa Kimaandiko katika mambo yote. Alisema, “Sasa, Neno la Mungu linasema, ya kwamba, ‘Neno liliwajilia manabii.’ Nanyi mliwaita wao ‘miungu,’ kwa maana Neno la Mungu liliwajia.” Kasema, “Basi mtanihukumuje ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?” Kwa torati yao wenyewe, Yeye aliwashona. Haya basi. Unaona?

258 Sasa tuko wapi? Tuko katika wakati wa mwisho. Sasa sikilizeni kwa makini sana sasa.

259 Sasa tunaona ya kwamba kungekuwa na vita na matetesi ya vita. Na sasa tunaona ya kwamba mtini umechanua majani yake. Na miti hiyo mingine imechanua majani yao. Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, na kadhalika, wamechanua majani yao, uamsho mkuu unaendelea.

260 Sasa ninaamini ya kwamba Mungu anamkusanya Bibi-arusi kwa ajili ya ile saa ya mwisho, walio Wateule. Loo, jamani! Sasa angalia.

261 Hebu sasa na tutafakari yale Yohana aliyoota, basi, kuhusu mambo haya aliyoota. “Farasi mwekundu; na mpandaji wake anaondoka, anapewa mamlaka kuua kwa upanga mkubwa.” Sasa huu hapa ufunuo wangu wa jambo hili. Huyu ni Shetani, tena. Ni Ibilisi, tena, katika umbo lingine. Sasa, tunajua ya kwamba—ya kwamba Mihuri ilihusu. . . kama nilivyosema juzi usiku. Na baragumu zinahusiana na vi—vi—vita vya wenyewe kwa wenyewe, unaona, miongoni mwa watu, miongoni mwa mataifa. Lakini unaona, hapa, ya kwamba mtu huyu ana upanga, kwa hiyo anahusiana na kanisa, vita vya kisiasa. Sasa huenda usifikiri hivyo, lakini angalia tu jambo hilo kwa dakika moja, dakika chache tu.

262 Angalia badilisho la rangi la farasi hawa. Mpanda farasi yule yule; badiliko la rangi ya farasi. Na farasi ni mnyama. Na mnyama, katika Biblia, chini ya mfano fulani, anawakilisha nguvu. Ni utaratibu ule ule ukipanda farasi wa rangi nyingine, nguvu, kutoka nyeupe isiyo na hatia mpaka aliye mwekundu kama damu. Unaona? Mwangalieni sasa, jinsi anavyokuja.

263 Wakati alipoanza mara ya kwanza, yeye alikuwa ninii tu, vema, alikuwa ni fundisho dogo tu katika—katika, miongoni mwao, lililoitwa unikolai. Bila shaka, haungeweza kuua cho chote. Hiyo ni Ufunuo 2:6, kama mkitaka kuliandika. Yeye hangeua cho chote. Ni fundisho tu, ni roho fulani tu miongoni mwa watu. Sasa, yeye hangeua cho chote. Loo, alikuwa asiye na hatia kabisa, akimpanda farasi huyu mweupe. “Vema, unajua, tunaweza kuwa na kanisa kubwa la ulimwenguni kote. Tungeweza kuliita kanisa la ulimwengu mzima.” Wangali

wanaliita hivyo. Vema. Unaona? Sasa, “Tungeweza kuwa na ninii. . .” Loo, halina hatia kabisa. Na, loo, halina hatia kabisa. “Ni kundi tu la watu. Tutaungana sote kwa ajili ya ushirika.” Unaona, hana hatia kabisa; ni mweupe, alikuwa ni farasi mweupe. Unaona?

<sup>264</sup> Sasa, kwa hiyo watu mashuhuri, na waliovalia vizuri, na wenye elimu, unajua, kwa namna fulani kama kila-ndege-nawimbile, unajua, “Kwa namna fulani tuta—tutaweka mambo pamoja. Na lile kundi lililo maskini, mbona, kama wanataka kuja wajaribu, vema, sawa, lakini sisi—tutataka kupata watu wa tabaka bora watakaohudhuria kanisa letu. Kama tunaweza tu kujitoa hapa, tuta—tutakuwa ninii—tutakuwa kundi la Wamasoni, ama kadhalika, unajua. Tuta—tutarekebisha tu mambo, ama, Shirika la Kusaidiana,” kama yanavyoitwa. Na kwa hiyo basi. . . Si Chama cha Kusaidiana sasa, lakini mnajua ninalomaanisha. Kwa hiyo, ni jambo geni kwa mwamini wa kweli. Sasa, lakini, vinginevyo, kwa maneno mengine, “Tunataka kundi dogo, shirika dogo tunaloweza kuliita letu wenyewe.” Ni fundisho fulani tu, halina hatia kabisa. “Ndugu, mbona, sisi hatuna kitu dhidi yenu ninyi watu, hashu. Ninyi hamna neno, lakini, mwajua, tunajisikia ya kwamba—ya kwamba tuna shughuli na kila nini hii. . . Sisi, tungekuwa na hali bora zaidi kama tulikuwa tumeungana pamoja.” Unaona? Hatimaye iliendelea moja kwa moja mpaka jambo hilo likatukia, naam, bwana, kuungana.

<sup>265</sup> Lakini wakati roho hii mbaya sana, ya udanganyifu (loo, jamani!) ilipofanyika mwili, katika roho iliyofanyika mwili; roho hii ya fundisho ilifanyika mwili, kupachukua mahali pa Kristo, katika mwanadamu. Haina budi kuabudiwa, halafu, iligeuka iabudiwe kama Kristo. Kwa maneno mengine, huko katika Vatican. . . Nilikuwa huko moja kwa moja. Imeandikwa, “VICARIVS FILII DEI,” na imeandikwa katika hesabu za Kirumi. Sasa chora tu mstari chini ya hizo herufi za Kirumi. Na inamaanisha, “Badala ya Mwana wa Mungu.” Yeye, kwa maneno mengine, yeye ni halifa. Mnajua halifa ni nini; ni kuchukua tu mahali pa kitu fulani. Yeye ni halifa, “Badala ya Mwana wa Mungu.”

<sup>266</sup> Na Biblia ilisema, “Yeye aliye na karama ya hekima na azihesabu hesabu za huyo mnyama, kwa kuwa ni hesabu ya mwanadamu. Na namba yake ni mia sita sitini na sita.” Sasa, hebu chukua VICARIVS FILII DEI, na uchore mstari, kwa namba za Kirumi; hiyo “V” badala ya 5, na “I” badala ya moja. . . Na ujumlishe, na uone kama hujapata mia sita sitini na sita.

<sup>267</sup> Biblia ilisema, “Atakuwa akiketi katika hekalu la Mungu, akiabudiwa kama Mungu.” Wakati fundisho hilo dogo lilipochukua mwili, akawa halifa, “Badala ya Mwana wa Mungu.” Unaona? Loo, jamani! Huyu roho mbaya sana,

mdanganyifu! Kama ukitaka kusoma jambo hilo, lisome katika Wathesalonike wa Pili 2:3, na unaweza kuona mahali jambo hilo lilipo.

268 Na, bila shaka, mtakumbuka Shetani ndiye kichwa cha mamlaka zote za kisiasa, za kila taifa. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnataka kuandika jambo hilo? Mathayo 4:8, “Shetani alimchukua Yesu juu ya mlima mrefu, na kumwonyesha falme zote za ulimwengu, zilizopata kuwapo ama zitakazopata kuwapo, katika dakika moja.” Nena kuhusu mtu! Akasema, “Nitakupata hizo, kama utaniabudu.” Naye Yesu alijua atakuwa mrithi wa hizo.

269 Hivyo ndivyo wanavyosema, “Loo, enyi kundi la maskini watakatifu wanaojivingirisha!”

270 Mbona, tutaupata ulimwengu! “Wapole watairithi nchi.” Hivyo ndivyo alivyosema Yesu. Unaona? Unaona?

271 Angalia, Yesu alijua Yeye angezirithi, kwa hiyo akasema, “Nenda zako, Shetani. Imeandikwa,” akarudi moja kwa moja kwenye Maandiko tena, unaona, “Utamwabudu Bwana, peke Yake.” Unaona?

272 Sasa—sasa wakati—wakati yeye, kwa kuwa yeye ndiye pepo mkuu, atakapofanyika mwili katika mtu huyu mkuu, wa kidini, kama vile Biblia inavyobashiri, ndipo anaunganisha kanisa lake na taifa. Nguvu zake zote mbili zinaungana pamoja. Unaona?

273 Wakati roho ya mpinga-Kristo ilipotoka ikaenda, ilikuwa ni roho. Halafu ikawa nini? Ikawa basi. . . Sasa angalia Muhuri huu. Wakati roho alipotoka akaenda, alikuwa ni mpinga-Kristo, dhidi ya mafundisho ya Kristo. Vema. Ndipo jambo lingine lililotukia. . . Yale Kristo aliyoliagiza Kanisa Lake liende kufanya, ilikuwa ni kupinga dhambi. “Loo, simaanishi jambo hilo. Simaanishi jambo hilo. Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya mtu mwingine. Hilo, hilo ni huko nyuma miaka mia iliyopita, kule nyuma. Hilo, hilo si kwa ajili yetu.” Unaona? Hilo, unaona, *pinga*, “dhidi.” Ndipo ikawa. . .

274 Sasa, yule mpanda farasi alitoka akaenda zake, ha—hakuwa na taji yo yote, lakini alipewa moja. Yule farasi mweupe; alikuwa na uta, bila mishale. Unaona? Kwa hiyo basi wakati alipotoka akaenda zake. . .

275 Ndipo, baada ya kitambo kidogo, alipewa taji, kwa sababu huwezi kuweka taji juu ya kichwa cha roho. Lakini, wakati, huyu roho alipofanyika mwili katika kazi ya pili ya ninii yake—ya kipindi chake cha wakati wa siri zake, kazi ya pili, alivikwa taji, nabii wa uongo, kwa ajili ya kutenda kazi kwa roho wa mpinga-Kristo. Sasa, tunamwona sasa, sasa. Sasa anakuwa hivyo, anapochukua hiyo. Halafu, yeye, tayari, ni Shetani anatawala nguvu za siasa za ulimwengu.

276 Sasa anafikia mahali hata atakuwa ni nguvu za kanisa la ulimwengu, akichukua nguvu za kidini. Na je! hivi hamfahamu, ndugu zangu, ya kwamba, katika . . . Wakati, taifa hili linapoonekana katika sura ya 13 ya Ufunuo, huyu mnyama mdogo aliyeinuka kama mwana-kondoo. Naye ana pembe mbili, nguvu ya kiserikali na kidini, lakini alifanya jambo lile lile huyo mnyama aliyemtangulia alifanya mbele zake.

277 Ni ajabu, Marekani ni namba kumi na tatu, na ni mwanamke. Ni ajabu, inapatikana hata katika sura ya 13 ya Ufunuo. Tulianza na milia kumi na mitatu katika bendera, nyota kumi na tatu. Kila kitu ni “kumi na tatu, kumi na tatu, kumi na tatu, kumi na tatu,” kote kote. Kila kitu ni “mwanamke, mwanamke, mwanamke,” kabisa kabisa.

278 Na hatimaye litaishia, (ninabashiri), mwanamke atalitawala. Kumbuka, hiyo ilikuwa ni miaka thelathini iliyopita, niliposema jambo hilo. Na—na yale—yale mambo saba niliyobashiri, matano yao yametimia. Nao wana mtu huyo papo hapo sasa wa kumwingiza mwanamke huyo. Nanyi mlimpigia kura, kwa siasa zenu pale. Naam. A-ha! Vema.

279 Kuna mengi sana ya kusema, ni vigumu kufikia mahali unapotaka kufikia. Sasa angalia. Sitawaweka ila kwa muda kidogo zaidi, kama itanibidi niendeleo kesho usiku.

280 Tazama. Angalia. Wakati Shetani. . . Sasa, kila mtu, ambaye, anatambua ya kwamba Shetani anatawala nguvu zote za siasa za ulimwengu. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye alisema hivyo. Mathayo mlango wa 4, mtalipata, na kifungu cha 8. Falme zote ni zake. Hiyo ndiyo sababu wanapigana, wanapigana vita, wanauana. Sasa kumbuka.

281 Je! jambo hilo si ni la ajabu? Walipewa upanga huu, wapate kuuana. Loo, loo, loo, jamani! Angalia sasa.

282 Sasa, wakati alipofanya jambo hilo, hakuwa na nguvu za kidini bado. Lakini alianza na pepo la mafundisho ya uongo. Na mafundisho hayo yakawa kanuni. Kanuni hiyo ikafanyika mwili katika nabii wa uongo.

283 Na basi akaenda moja kwa moja mahali penyewe kabisa. Hakuenda Israeli, sasa. Alienda Rumi; Nikea, Rumi.

284 Walifanya baraza, nao wakachagua askofu mkuu. Na ndipo, kwa kufanya jambo hili, waliunganisha kanisa na taifa pamoja. Ndipo, akaangusha uta wake. Akashuka kwenye farasi wake mweupe. Akampanda farasi wake mwekundu, kwa maana anaweza kuua mtu ye yote asiyekubaliana naye. Huo hapo Muhuri wako. Jamaa yule yule! Mwangalie akipanda akielekea huko Umilele, pamoja naye, unaona, anaunganisha nguvu zake mbili pamoja.

285 Ni jambo lile lile wanalojaribu kufanya sasa hivi, jambo lile lile, leo. Na jambo la ajabu, labda hufahamu jambo

hilo. Lakini, leo, kutoka katika kundi la Kibaptisti huko Louisville. . . Mlisikia jambo hilo kwenye redio. Mnenaji mmoja alisimama na. . . Ni wangapi waliosikia jambo hilo? Kweli. Unaona? Vema, haya basi. Wao wanataka, na waliomba kanisani sasa, ya kwamba haitubidi hasa, kuninii, loo, kwa namna fulani tu kujiunga na kanisa Katoliki, lakini itatubidi kwa namna fulani kuwa na ushirika pamoja nao. Kupata. . . Na, wakati uo huo jambo hilo linapoendelea kule Louisville, upande huu Mungu anawafunulia watu Wake Mihuri, kuonyesha jambo hilo, “Msifanye hivyo!” Mnawaona hao wawili wakifanya kazi pamoja? Kumbukeni, kunguru na hua waliketi kwenye kijiti kile kile cha kutulia, katika safina. Hakika. Kumbukeni tu.

<sup>286</sup> Sasa tunaona, anaunganisha nguvu zake, basi, wakati alipokuwa taifa na kanisa pia, serikali ya kanisa. Basi utafanya nini? Anaunda dini yake mwenyewe. Na sasa anaweza kufanya lo lote analotaka kufanya. Basi, ana haki ya kuuu mtu ye yote asiyekubaliana naye. Hivyo ndivyo alivyofanya kabisa, pia. Na hivyo ndivyo alivyofanya hasa. Na kile yeye—yeye. . . Aliwafanya hivyo watakatifu wa Mungu aliye hai, walidumu na Neno wala hawangekubaliana naye juu ya mafundisho yake ya sharti. Aliwaua.

<sup>287</sup> Sasa, Ndugu Lee Vayle, na ninyi waalimu hapa wa wakati wa Nikea na kanisa la mwanzoni, mimi sijui kama mlisoma jambo hili ama hamkulisoma. Kama mnataka kulisoma, linapatikana katika kitabu cha Schumucker kinachoitwa *Glorious Reformation*.

<sup>288</sup> Nanyi unaona jambo hilo, ya kwamba, wakati Mtakatifu Augustino wa Hippo alipokuwa kasisi chini ya kanisa la Roma, alipata nafasi, hata wakati mmoja Roho Mtakatifu alitaka kumshukia, naye akamkataa. Ni wangapi wanajua jambo hilo, kama mwalimu? Kwa hiyo, yeye alimkataa Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo ilivyo hasa, mfano wa kanisa la Kiprotestanti leo, ambalo limemkataa Roho Mtakatifu. Alirudi huko Hippo, naye ndiye mwenyewe hasa aliyetia sahihi ile, ile karatasi iliyosema, “Ufunuo kutoka kwa Mungu, ya kwamba ilikuwa ni sawa na inampendeza Mungu, kumwua kila mtu ambaye hakuamini pamoja na kanisa la Romani Katoliki.”

<sup>289</sup> Sasa sikilizeni. Ninanukuu kutoka kwenye kitabu cha wafia imani, “Tangu wakati wa—wa Mtakatifu Agostino wa Hippo, mpaka 1586,” kwenye kitabu cha wafia imani wa Roma, “kanisa la Romani Katoliki liliwaua Waprotestanti milioni sitini na nane.” Je! upanga wake ulikuwa mwekundu? Je! alikuwa amempanda farasi mwekundu? Ilikuwa ni nini? Nguvu zile zile; mpanda farasi yule yule. Huo hapo huo Muhuri. Wao wanakubali, “milioni sitini na nane,” kwenye kitabu cha wafia imani, mbali na wale wote waliouawa nje ya hao. Loo, rehema! Katika wakati wa nyakati za giza, kulikuwako na mamilioni waliolishwa kwa simba, na kuuawa kwa kila njia, kwa sababu

wasingekubali fundisho hilo la sharti la Katoliki. Mnajua jambo hilo.

<sup>290</sup> Mna wakati gani umebakia? [Kusanyiko linasema, “Wakati mwingi sana. Usiku kucha.”—Mh.] Vema. Hebu nisome jambo fulani. Tufungue sasa, hebu niwaonyeshe jambo fulani. Hebu—hebu na tuangalie jambo hili, kwa dakika moja tu. Imetokea kwamba nimelikumbuka sasa hivi, nasi tutalisoma tu. Hebu na tufungue Ufunuo, sura ya 17 ya Ufunuo. Tungali tuna dakika kumi na tano zilizosalia. Vema. Sasa sikilizeni kwa makini sana, sana sasa, tunaposoma. Ninyi mlio na Biblia zenu na mfungue, nitawapa tu muda kidogo, ili kwamba mlipate.

<sup>291</sup> Je! ulilipata hilo, Lee? Nimelipata kwenye kitabu cha Schmucker, unaona, *Glorious Reform*, hilo lilichukuliwa moja kwa moja kutoka kwenye kitabu cha wafia imani cha Rumi, huko Vatican.

<sup>292</sup> Sasa, hiyo ilikuwa ni kufikia mpaka kwenye yale mateso ya watu wa Mtakatifu Patriki. Na halafu eti wao wanamwita Mtakatifu Patriki mtakatifu wa—wao. A-ha! Mtakatifu Patriki alikuwa Mkatoliki kulingana tu kama vile mimi nilivyo; nanyi mnajua mimi ni Mkatoliki jinsi gani. Unaona? Yeye—yeye alilichukua sana fundisho la kanisa hilo. Alikataa kwenda kwa papa. Ndivyo, bwana. Mtakatifu Patriki hata . . . Mbona, ninyi, je! mlipata kwenda huko Ireland ya Kaskazini, ambako alikuwa na shule zake? Mnajua, jina lake halikuwa Patriki. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Jina lake lilikuwa ni Sukati. Hiyo ni kweli. Alimpoteza dada yake mdogo. Mnakumbuka wakati wao . . . Unaona? Vema.

<sup>293</sup> Sasa angalia, mlango wa 17 wa Ufunuo. Sasa kila mtu na ajaribu kufungua moyo wake. Hebu Roho Mtakatifu na akufundishe sasa.

*Akaja kwangu mmoja wa wale malaika saba, wenye—  
wenye vile vitasa saba, . . .*

<sup>294</sup> Sasa, unaona, kuna vile Vitasa Saba. Uwajua, hizi saba, wakati tunapopitia, zote zinatukia wakati ule ule; kufuatana na yale Mapiyo, vikifuatana na nyakati za kanisa, vile vile tu, kwa sababu yote yametiwa muhuri katika kile Kitabu kimoja, kila kitu. Na kila kitu kinatukia katika mzunguko tu; kimoja kinaingia moja kwa moja katika hicho kingine, na hicho kingine, na hicho kingine. Kuna roho mbili zinazofanya kazi; Mungu, na Ibilisi. Unaona?

*. . . wenye vile vitasa saba vya mwisho, na akanena  
nami, akisema, . . . Njoo huku, nami nitakuonyesha . . .  
hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji  
mengi;*

<sup>295</sup> Sasa angalia hapa, huku, hayo, “maji.”



296 “Kahaba,” hicho ni nini? Huyu ni mwanamke. Hawezi kuwa ni mwanamume. Na mwanamke anaonyeshwa na kitu gani kanisani, katika Biblia? Kanisa. Kwa nini? Bibi-Arusi wa Kristo, na kadhalika; unaona, ni mwanamke, kanisa.

297 Sasa, “maji,” hayo yana maana gani? Angalia hapa. Soma kifungu chake cha 15 hapo.

*Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa...makutano...mataifa na lugha.*

298 Kanisa hili lilikuwa likitawala ulimwengu mzima, unaona, “Aliyeketi juu ya maji mengi.”

*Ambaye wafalme wa nchi wamezini naye, uzinzi wa kiroho (kuchukua fundisho lake, fundisho la Wanikolai), nao wakaa katika nchi wamelevywa kwa mvinyo ya uasherati wake.*

299 Jamani, unanena kuhusu kundi lililolewa, kwa hilo! Wewe...

*Basi akanichukua katika Roho hata jangwani, na nikaona mwanamke,...*

300 Na je! ulijua nini? Vitabu vyenyewe vya Wakatoliki vinakubali kwamba hili ni kanisa lao. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Kwenye vitabu vyao wenyewe kabisa. Nina *Facts of Our Faith*, kinavyoitwa, sasa, unaona; ni cha kasisi fulani. Vema. Vema.

*Na kwa hiyo akanichukua katika Roho hata jangwani, na nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana, mwenye kujaa majina ya makufuru, mwenye vichwa saba na pembe kumi.*

301 Sasa angalia tu jambo hilo, ishara hiyo, hivyo “vichwa saba.” Sasa unaona hapa mahali iposemwa, “Na vile—na vile—na vile...Vile vichwa ulivyoviona ni milima saba anapoketi mwanamke huyo.” Rumi imekaa juu ya milima saba. Unaona? Sasa hakuna kosa kuhusu jambo hilo, unaona, “Vichwa saba.” “Na pembe kumi,” unajua, ni zile falme kumi, na kadhalika.

*Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau,...nyekundu, amepambwa katika dhahabu, na kito cha thamani, ...na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na chukizo—chukizo, la machafu ya uasherati wake.*

302 Ie roho ya mpinga-Kristo, “uasherati,” unaona, “mafundisho,” hiyo ni kufanya usinzi juu ya Mungu. Unaona? Sasa, yeye anapaswa kuwa Bibi-Arusi, unaona; na anafanya uzinzi. Unaona? Kama tu vile Hawa alivyofanya, kama tu vile kanisa linavyofanya pale. Unaona?

*Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, LA SIRI, BABELI MKUU, . . .*

303 Na mtu ye yote anajua, “BABELI” ni Rumi.

*. . . MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.*

304 Basi sikiliza kifungu cha 6.

*Na nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu. Nami nilipomwona nikastajabu ajabu kuu.*

305 Alikuwa ni kitu cha kupendeza sana, akiwa na misalaba na kila kitu juu yake! “Anawezaje kamwe kuwa na hatia ya kulewa kwa damu ya watakatifu?” Lilimshangaza. Sasa atamwambia.

*Na yule malaika akaniambia, Kwani kustajabu? Nitakuambia siri ya mwanamke huyu, na . . . mnyama huyu aliyemchukua, . . .*

306 Sasa, hili haliko chini ya moja ya ile Mihuri. Hili ni jambo lingine, unaona.

*Naye akasema . . . vile vichwa saba na zile pembe kumi.*

*Yule myama uliyemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu (hana msingi, papa), na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi, wasiondikwa majina yao katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, (hao hapo wateule, unaona), uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, . . .*

307 Ni vipi, ni lini jina lako lilipoandikwa katika Kitabu cha Uzima? Kwenye ule uamsho uliohudhuria? La, bwana. “Tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

*. . . watastajabu walipomwona yule mnyama, ya kwamba alikuwako, . . . hayuko, naye atakwako.*

308 Unaona, “yule mnyama,” mmoja atakufa, mwingine atachukua mahali pake. “Alikuwako; hakuwako. Alikuwako; hakuwako. Alikuwa; hakuwako.” Naye ataenda moja kwa moja mpaka kwenye uharibifu, namna hiyo. Unaona? Vema.

*Na hapa ndipo penye—na hapa ndipo penye akili zenye hekima.*

309 Ni wangapi wanaojua kuna karama tisa za kiroho, na moja ya hizo ni hekima? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Vema.

*Vile vichwa saba ni milima saba anayokalia mwanamke huyo.*

310 Loo, itabidi uwe u kipofu kabisa, kiziwi na bubu, usilipate jambo hilo. Unaona? Vema.

*. . . kuna wafalme saba. Watano wamekwisha kuanguka, na mmoja yupo (Nero), na . . . mwingine*

anakuja. *Naye atakapokuja imempasa kukaa muda mchache tu.*

311 Unakumbuka yale aliyofanya. Aliuteketeza mji, na akawasingizia Wakristo. Na akamweka mamaye kwenye mti mmoja wa farasi na kumkokota mitaani. Ndipo akacheza fidla, wakati Rumi inateketea. Vema.

*Na yule mnyama aliyekuwako naye hayuko, yeye ndiye wa nane, . . .*

312 Rumi ya kipagani, ilifanywa kuwa Rumi ya papa. Wakati roho ya mpinga-Kristo ilipofanyika mwili, na akavikwa taji, alivikwa taji kama mfalme wa Rumi, wa taifa na wa kanisa pia, pamoja. Loo, ndugu! Unaona, hiyo imejaa mambo hayo tu. Unaona?

*. . .ni . . .wa saba, naye anaenda . . .(Yeye anadumu muda gani? Wao hawabadilishi utaratibu huo.) . . . kwenye uharibifu.*

*. . .zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, ambao hawajapokea falme za wafalme bado, lakini wapokea mamlaka kama wafalme muda wa saa moja pamoja na yule mnyama.*

313 Hao ni watawala wa mabavu, unaona, bila shaka. “Hawa wana nia moja.” Sasa angalia hapa. Haizungumzii juu ya ukomunisti. Unaona?

*Hawa wana shauri moja, nao wanampa yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao.*

*Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana-Kondoo atawashinda, kwa maana Yeye ni Bwana wa bwana, na Mfalme wa wafalme; na hao walio pamoja naye ndio walioitwa, . . .wateule, na waaminifu.*

*Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa . . .makutano . . .mataifa na lugha.*

*. . .zile pembe kumi ulizoziona, juu ya huyo mnyama, hao watamchukia yule kahaba, na agano hilo limevunjwa . . .(nilizungumza juu ya jambo hilo jana usiku.) . . .nao watamfanya kuwa mkiwa na uchi, na watamla nyama yake, na watamtekeza kabisa kwa moto.*

314 Hivi hujui Biblia inasema ya kwamba manahodha, na cho chote kile kinginecho, walisema, “Ole, ole, mji ule ulio mkuu! Jinsi ulivyopata hukumu yake katika saa moja!” Unaona?

*Maana Mungu ametia mioyoni mwao kufanya shauri lake, na kufanya shauri moja, na kumpa yule mnyama falme zao hata neno la Mungu litimizwe.*

*. . . yule mwanamke uliyemwona ni mji ule mkubwa,  
wenye ufalme juu ya wafalme wote wa nchi.*

315 Niambie mmoja. Urusi haitawali juu ya wote. Sisi hatutawali juu ya wote. Kuna mfalme mmoja tu anayetawala juu ya kila . . . kama kile chuma cha Nebukadreza kinachopita katika kila kimoja cha hivyo vidole vya miguu. Hicho ni Rumi. Rumi haifanyi jambo hilo kama taifa; inafanya hivyo kama kanisa. Kila taifa chini ya mbingu liko chini ya Rumi.

316 Si ajabu wao walisema, “Ni nani anayeweza kufanya vita naye?” Yeye anaweza kusema, “Amani,” [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.] hilo linatosha. Kila Mkatoliki aseme, “Ni ninii, ‘Msipigane,’” na—nao hawatapigana. Hilo tu basi. “Ni nani anayeweza kufanya yale anayoweza kufanya?” Hakuna. Hiyo ni kweli. “Kwa hiyo wanashangazwa na miujiza anayoweza kufanya.” Anaweza kusimamisha vita. [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja.] Jambo tu linalompassa kufanya ni kusema tu, “Msipigane.” Hilo tu basi. Lakini unafikiri atafanya hivyo? Hawezi kamwe.

317 Angalia, hiyo kweli inaonyesha, “Watauana. Watauana.” Uta wake haukuwa na mishale, kwanza, lakini “upanga wake mkuu” uliua. Alifanya mauaji yake, baadaye, na akabadili kutoka farasi mweupe na akampanda farasi mwekundu; ni Ibilisi, yule yule, hasa, na upanga wake.

318 Yesu alisema nini? Yesu alisema, “Wale waushikao upanga wataangamia kwa huo.” Usipigane. Unaona? Yesu, usiku huo wakati alipomwambia, aliposema jambo hilo, na Petro akautwaa upanga wake. Unaona? Wewe fanya tu kama Yeye alivyofanya, songa mbele tu.

319 Sasa, sasa kumbukeni, yeye ana upanga. Anatoka kwenda mbele, upanga mkononi; amepanda, farasi mwekundu, akikanyaga na kupitia katika damu ya kila mtu asiyekubaliana naye.

320 Sasa mnafahamu jambo hilo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Ni wangapi wanaofahamu Muhuri huo ni nini sasa? [“Amina.”] Vema. sasa, Yesu alisema nini? “Waushikao upanga wataangamia kwa upanga.” Hiyo ni kweli? Vema. Vema. Mpanda farasi huyu na raia wote wa ufalme wake wanaoua katika ule wakati wote mzima, ambao wamemwaga damu hii yote ya wafia imani ya watakatifu, watauawa kwa Upanga wa Yesu Kristo hapo atakapokuja. “Hao waushikao upanga watauawa kwa upanga.” Waliuchukua upanga wa fundisho la sharti na la mpinga-Kristo, na kuwaua waabudu halisi, wa kweli, kote kote katika nyakati, kwa mamilioni. Na wakati Kristo atakapokuja na ule Upanga, kwa maana ni Neno Lake linalotoka katika kinywa Chake, Yeye atamwua kila adui aliyeko mbele Zake. Mnaamini jambo hilo? “Kumwua yule adui.”

321 Hebu na twende hapa kwa dakika moja tu, Ufunuo. Tutaona sasa kama mimi ninasema tu jambo hilo, ama kama Neno linalisema. Ufunuo 19:11.

*Kisha nikaona mbingu zimefunuka (amina), na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda, anaitwaa Mwaminifu na Wa-Kweli, naye kwa haki amehukumu na kufanya vita.*

*Macho yake yalikuwa . . . miali ya moto, na juu ya kichwa chake . . . vilemba vingi; . . .*

322 Loo, ndugu! unaona, Yeye tayari amekwisha kuvikwa taji na watakatifu Wake, unaona.

*. . . naye ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu ila . . . mwenyewe.*

323 Kumbukeni, ha—hatuwezi, hatulijui hilo, unaona, ni lipi. “Naye alikuwa amevikwa . . .” Hebu tuone.

*Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na jina lake aitwa (si “ni,” lakini “aitwa”), Neno la Mungu.*

324 Kwa kuwa, Yeye na Neno ni mmoja. Unaona? Sasa angalia, si “Majina Yake.” A—ha! “Jina Lake anaitwa ‘Neno la Mungu.’” Inajua tu Jina moja; hakuna jina lingine.

*Na majeshi ya mbinguni yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi. (Hiyo ni haki ya watakatifu. Unaona?)*

325 Sasa angalia. Yesu alisema nini? “Yeye aushikaye upanga . . .” Vema, mpanda farasi mwekundu, hapa ambapo anakuja. “Yeye aushikaye upanga . . .” Huenda uliwaua milioni sitini na nane wa hao, kote kote katika nyakati hizi zote, tangu wakati huo; labda zaidi. Lakini Yesu alisema, “Yeye aushikaye upanga ataangamia kwa huo.” Angalia.

*Na upanga mkali hutoka kinywani mwake, . . .*

326 Waebrania, sura ya 4, ilisema, “Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, unakata hata kwenye mafuta ya viungo.” Na linafanya nini, hilo Neno, linafanya nini? “Ni tambuzi la mawazo ya moyo.” Kweli.

*. . . upanga mkali ukatao kuwili . . . upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi.*

*Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA MFALME, NA BWANA WA MABWANA.*

327 Kama wadanganyifu, dhidi ya Neno la Mungu, na kwa sababu wasingekubali, na jambo hili . . . Shetani aliweka,

uliunganisha nguvu za kisiasa alizokuwa nazo, na nguvu za kiroho alizokuwa nazo, pamoja, na kuunda kanisa linaloenea katika kila taifa. Naye ameuua mamilioni mara mamilioni... baada ya kuruka kutoka katika farasi wake mweupe, akapanda farasi wake mweupe, naye akautwaa upanga wake na akatoka kwenda zake.

328 Lakini Mungu alisema, “Kwa Kitu kile kile alichopotosha, au alichotaribu kupotosha, kwa mafundisho ya uongo; Neno lilo hilo litainuka katika nguvu, likitoka katika kinywa cha Yesu Kristo, nalo litamwua, na kila kitu kilicho mbele Zake.” Amina.

329 Huo hapo Muhuri wa Pili. Mnampenda? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Loo, jamani! Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. [Kusanyiko linashangilia sana.] Mungu asifiwe! Kama mafunuo haya mengine yote, na maono, na kila kitu, huu umetimia ji—kikamilifu kweli kweli kabisa! Na ni wangapi wanajua jambo hilo? Inua mkono wako. Mamia, kila mtu hapa, wameinua mikono yao. Hiyo ni kweli. Vivyo hivyo Huu utatimia! Kumbukeni, ndio hivyo. Loo, ewe rafiki!

Njoo kwenye chemichemi iliyojaa Damu,  
Ibubujikayo toka kwenye mishipa ya damu ya  
Imanueli;  
Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa  
chini ya mto huo uliofurika,  
Wanaondolewa mawaa yao ya hatia.

330 Njoo, mwamini Yeye, kama hujapata kumwamini. Usibahatishe; usibahatishe, usibahatishe, kama kuna kitu cho chote maishani mwako, rafiki.

331 Tumewasili. Jambo fulani liko karibu na kutukia. [Ndugu Branham anapiga-piga mimbarani mara nne—Mh.] Sijui ni kwa nini. Sijui ni lini. Ninajua litakalotukia, lakini sijui ni lini litakapotukia. Lakini halina budi kuwa, kwa maana Yeye analifunua sasa hivi. Yeye hafanyi jambo lo lote pasipo kulifunua. Amosi 3. Yeye hulifunua, kwanza. Naye aliahidi ya kwamba mambo haya yatakuja katika siku za mwisho. Na ule wakati wa saba wa kanisa, mwisho wake, wakati mjumbe amewasili, hapo ingetimia. Ingefunuliwa, hiyo Mihuri iliyovunjwa itafunuliwa, na ndio Hii hapa. Sasa, hilo ni katika Jina la Bwana. Amini ni jambo Hilo, ewe rafiki. Naam, bwana. Tokeni Babeli!

332 Ninataka kusema jambo fulani kabla ya kufunga. Maana, nina... Inafikia kwenye saa tatu na nusu. Ni wakati unaofaa sasa.

333 Mimi na Billy, tuliposhuka kutoka kwenye ndege, huko India, safari yetu ya mwisho kule. Nilikuwa nikisoma ga—gazeti waliloleta, lilikuwa limeandikwa katika Kiingereza. Nalo lilisema, “Hapana budi tetemeko la nchi limekwisha; ndege

wanarudi.” Ndipo linaelezea kirefu. Wao . . . Kulikuwa na jambo la ajabu lilitukia.

334 India hawana fensi zilizofumwa kama tulizo nazo sisi. Wao wanaokota mawe, na kutengeneza fensi zao. Nao wanajenga nyumba zao nyingi kutokana na na mawe, wanayabandika tu hapo juu. Na kuna joto kule, kila mahali, loo, po pote pale, karibuni kote, kule India, isipokuwa uwe uko huko juu milimani. Na huko chini kote kupitia Calcutta na kadhalika, watu wanalala tu mitaani, wakifa kwa njaa, na kadhalika.

335 Sasa, kwa hiyo, na wanajenga nyumba zao katika minara, ya nyumba zao. Wanazitungushia fe—fensi moja kwa moja hapa, kuzunguka nyumba yao. Wanajenga mnara wa nyumba yao, na mnara unaweza kuwa pale walipochimba kisima chao. Wanakichimba kwa ajili ya ng’ombe wao na kadhalika, kisha wanavitungushia boma.

336 Na, mara, jambo fulani likaanza kutukia. Wale ndege wadogo, unawajua, wanaingia kwenye miamba hiyo, na kujenga viota vyao na kulea vifaranga vyao. Na jambo fulani likaanza kutukia.

337 Kila siku, kunapokuwa na joto, ng’ombe wote watakusanyika na kusimama chini ya kivuli cha kuta hizo; wapate upepo.

338 Na ndege wote wadogo wanaishi katika sehemu hizo mahali hapo. Na, mara, hao ndege wote wadogo, kwa sababu fulani isiyojulikana . . . Sasa, mnajua tuliyosema hivi majuzi kuhusu ndege wadogo. Unaona? Kwa sababu fulani isizojulikana wote, waliondoka. Nao wakatoka wakaenda zao, wala hawakurudi kwenye viota vyao. Walienda huko kondeni, wakaketi kwenye miti, na mahali po pote wangaliweza kupapata, ama moja kwa moja ardhini.

339 Ng’ombe hawangekaribia. Kondoo wasingekaribia. Walikaa moja kwa moja kondeni, na kuegemeana. Hilo ni jambo zuri la kufanya. Walijua kwamba jambo fulani litatukia.

340 Halafu, mara, tetemeko la nchi likatokea, na kuzitikisa kuta zikaanguka, na kuangusha fensi, na kila kitu.

341 Ndipo wale ndege wadogo wakaanza kurudi. Hawakurudi kwa yapata siku tatu ama nne; ndipo walipoanza kurudi. Wao wakasema, “Vema, matetemeko ya nchi hayana budi yamekwisha sasa; ndege wanarudi.”

342 Mbona? Je! hamwamini ya kwamba Mungu yeye yule ambaye angewafanya ndege na ng’ombe na kondoo, katika zile siku za Nuhu, waingie katika ile safina, angali ni Mungu yeye yule anayeweza kuwafanya waruke waende kwenye mahali pa usalama? Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

343 Sasa hebu niseme jambo fulani, ndugu. Kuna jambo fulani lililo karibu na kutukia. Na kuta hizi zote kubwa, za kale za

kidini zitaanguka, na kurudi kule ng'ambo, na kukubaliana. Maana, watafanya jambo hilo, hakika tu kama ninavyosimama hapa. Hiyo ndiyo "Sanamu ya yule yule mnyama," hakika tu kama ninavyosimama hapa; na taifa hili limeichukua, kulingana na Neno la Bwana. Sikilizeni, unaposikia hisi hiyo ndogo, ya ajabu, ondoka kwenye kuta hizo. Ondoka! Mtafia humo ndani. Msifanye jambo hilo! Tokeni kwake! Tokeni kwenye upuuzi huu wote! Kimbilieni kwenye usalama, upesi mwezavyo. Mwombeni Mungu rehema.

<sup>344</sup> Usichukue tu, baadhi ya, "Vema, mama yangu alikuwa ni Mmethodisti, kwa hiyo nadhani nitakuwa hivyo. Baba yangu alikuwa ni Mbatisti; nitakuwa hivyo." Usifanye hivyo. Usi—usibahatishe hata kidogo.

<sup>345</sup> Sijali linaonekana rahisi na nyenyekevu namna gani; ni Neno la Bwana. Kimbilieni kwa Yesu Kristo upesi mwezavyo, na ukae hapo mpaka Mungu atakapokujaza na Roho Wake Mtakatifu. Kwa sababu saa yaja wakati utakapomtafuta Huyo, wala hatakuwako. Kwa hiyo, hakikisheni mmempata.

Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa dakika moja.

<sup>346</sup> Baba wa Mbinguni, loo, ni—ninaninii tu, wakati mwingine, Bwana, ninasimama hapa na—na ninatetemeka. Ninafikiri juu ya ile saa ya kuogofya inayokaribia, nami . . . Hakuna njia ya kuizuia. Imetabiriwa itakuja. Nami nilifikiri juu ya, "Kwa nini watu hawaji na—na—na kusikiliza? Na mbona wasije na kulikubali?" Lakini, bila shaka, ninajua ya kwamba—ya kwamba Wewe—Wewe ulisema hawatalikubali, kwa hiyo hawatalikubali.

<sup>347</sup> Lakini kuna baadhi yao ambao majina yao yameandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Na wakati Mihuri hiyo inapofunguliwa wazi kule, wanaona majina yao mle, na Roho Mtakatifu ananena nao. Wanakuja. Huwezi kuwazuia; hakuna mtu anayeweza kuwazuia, hakuna hata mmoja. Wao wanakuja, kwa vyo vyote vile, kwa sababu Wewe unawaongoza kama ulivyowafanyia wale ndege wadogo, na kondoo na ng'ombe. Wewe ni Mungu! Silika fulani waliyo nayo hao wanyama, kwamba wanajua ya kwamba hawana budi kuondoka! Na kama silika, kwa mnyama, inaweza kumwonya aikimbie hatari, Roho Mtakatifu anapaswa kufanya nini kwa Kanisa linalodai limejazwa Naye!

<sup>348</sup> Mungu, uturehemu. Tusamehe sisi sote, Bwana, makosa yetu. Hatumaanishi kusimama hapa kwenye mimbara hii na kuwaacha watu hawa wasimame kando ya kuta, huku viungo vyao vya mwili vikiuma, na halafu waondoke waende zao tu na kusema, "Vema, hilo linasikika ni jambo zuri sana." Bwana, tunataka kufanya jambo fulani juu yake. Sisi, tunakutaka Wewe uichunguze mioyo yetu. Kama kuna jambo lo lote baya, Bwana, tujalie tujue sasa. Tafadhali usituache tuifikie ile saa,



huko ng'ambo, wakati tumeisha chelewa tayari. Nichunguze. Niangalie, Bwana.

<sup>349</sup> Hapa, ninasimama hapa kwa neema ya Mungu, nikiona Mihuri hiyo imevunjwa kule juu, nami naja, nikiwaambia watu. Wakati, Wewe ulibashiri lingetukia namna hii, majuma kadha yaliyopita. Na sasa, Baba, ndio Hili hapa, waziwazi mbele zetu.

<sup>350</sup> Sasa, Bwana, niangalie. Nichunguze. Nichunguze, moyoni mwangu. Bwana, sisi hatuninii...Sisi, tunakutaka Wewe uyachunguze maisha yetu. Na kama kuna jambo lo lote ndani humo, ambalo si sawa, tuambie tu, Bwana. Tunataka kulisahihisha, sasa hivi; sasa hivi, wakati kuna Chemchemi iliyojaa Damu, wakati kuna—kuna kitakasaji kinachoweza kusafisha dhambi zetu na kutokuamini. Tunataka kutumbukiza nafsi zetu chini ya hicho; kutokuamini kwetu kote. Mungu, tusaide kutokuamini kwetu; tuondolee kutokuamini, Bwana.

<sup>351</sup> Tunataka kupokea neema ya kunyakuliwa. Tunataka kuweza, wakati hiyo Ngurumo ya siri itakaponguruma huko ng'ambo, na Kanisa linatwaliwa juu, tunataka kuwa tayari kuipokea hiyo. Bwana, tujalie.

<sup>352</sup> Tuangalie, Bwana, kwa Neno Lako. Hebu na tulichunguze. Na kama tukiona ya kwamba tumepunguka...Kama kuna wale hapa, Bwana, waliokuwa wamebatizwa katika vyeo; wakiwa hawajui kitu kuhusu ubatizo halisi, wa kweli! Nijalie niwe mwaminifu kama Paulo...

<sup>353</sup> Wakati alipopitia kwenye pwani ya juu ya Efeso, naye akakutana na wanafunzi waliokuwa wakipiga makelele, na kupaza sauti zao, wakiwa na wakati mzuri sana. Yeye aliwaambia, "Je! mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" Hawajui kama yuko. Akasema, "Basi mlibatizwaje?" Nao walikuwa wamebatizwa na yule nabii mashuhuri, mtakatifu, lakini walibatizwa tu kwa toba. Ndipo wakabatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo. Naye Paulo akawaamuru wabatizwe, mara nyingine tena.

Bwana, katika Nuru ya Neno Lako!

<sup>354</sup> Ninamwamuru kila mtu, ambaye hajabatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, akimbilie majini, upesi, wakati mtu ukiwa una nafasi.

<sup>355</sup> Ninyi ambao hamjazwa na Roho Mtakatifu; ninawaamuru, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, nendeni magotini. Wala msiamke mpaka Roho Mtakatifu amewatakasa kabisa na kuwajaza na upendo na wema Wake; mpaka nafsi yako imeridhika sana mbele ya Uwepo wa Mungu, kwamba shauku yako yote ni kumtumikia na kumwishia Yeye, na kufanya kazi pamoja Naye, maishani mwako mwote.

<sup>356</sup> Tujalie. Ninaomba ya kwamba Mungu atakupa agizo hili, katika Jina la Kristo.

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza

Mnampenda kweli kweli? Sasa inueni mikono yenu juu.

Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

357 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.] Kama kuna ye yote anayeketi, wanaosikia haja yao usiku wa leo, wanaojisikia wanataka kubatizwa, ama wanaotaka ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unajua haja yako; imefunuliwa kwako, nawe unataka kukumbukwa katika maombi. Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kukupa Huyo. Loo, tunaweza kukubatiza. Lakini, kitu kimoja, sisi hatuwezi kukupa Roho Mtakatifu. Mungu hufanya jambo hilo, peke yake. Lakini ulihisi haja yako, ya kwamba Mungu ananena na moyo wako, ya kwamba unamhitaji Yeye, na unataka tukukumbuke katika maombi. Unaweza kusimama, ili tupate kukujua, kujua wewe ni nani? Mungu na akubariki. Haja? Bwana akubariki.

358 Ninadhani kuna mia na hamsini, labda, wanaosimama hapa. Labda ni kiasi hicho, kama ningeweza kuwaona wote. Sijui huko kwenye vyumba, na huko nje, walioinua mikono yao juu, na kadhalika. Lakini una haja.

Sasa hebu na tuombe.

359 Sasa, ninyi mnaowaona watu hao wanaosimama karibu nanyi. Nao wanasimama kama shahidi, mbele za Kristo, “Ni—ni—ninakuhitaji Wewe, Bwana. Ninakuhitaji. Ni—ninaamini mimi—mimi ni mmoja wa hao ambao wataona jina langu usiku wa leo nyuma ya ule Muhuri kule ng’ambo, lililoandikwa Mle tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kitu fulani kiliugusa moyo wangu, nami ninasimama, Bwana. Je! ni mimi? Je! unaniita? Ninataka unifunulie, mimi, jina langu Kule. Nijaze, na unitie muhuri ndani Yako, kwa Roho Mtakatifu.” Ninyi ambao tayari mmetiwa muhuri ndani, ninawatakeni msimame. Wageukieni, na mwawekee mikono, kuwaombea. [Ndugu Branham anatulia.] Sasa iweni waaminifu sana. [Kusanyiko zima linaanza kuomba—Mh.]

360 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, jalia Roho Mtakatifu aliye mkuu atende kazi kwenye kusanyiko hili, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, na kuuita kila moyo hapa, Bwana. Na aushushe ubatizo wa Roho Mtakatifu, juu ya watu hawa.

Na kuna maji yanayongojea.

361 “Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu alikawashukia wale waliolisikia lile Neno, nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu.”

[Kusanyiko zima linaendelea kuomba—Mh.]



*UFUNUO WA MIHURI SABA*  
(The Revelation Of The Seven Seals)

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kutoka tarehe 17 Machi mpaka tarehe 24 Machi, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, na Muhuri wa Saba ukaendelea tarehe 25 Machi katika Hoteli ya Sherwood. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamilifu zaidi, kitabu hiki kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jitihada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

Haki zote zimewekwa. Kitabu hiki hakiwezi kuuzwa, kuchapishwa tena, ama kufasiriwa katika lugha zingine, ama kutumiwa kwa kuchangisha fedha bila barua ya kuruhusia ya William Branham Evangelistic Association. Kilichapishwa tena katika mwaka wa 2006.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)